# JARIDA LA MKOA WA RUVUMA

## SEKTA YA AFYA KATIKA MKOA WA RUVUMA




**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA**

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI OFISI YA MKUU WA MKOA WA RUVUMA**

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigachapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya mwandishi kwa maandishi.

Jarida limehaririwa na Albano Midelo wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

Limesanifiwa na kupigwa chapa na

**YALIYOMO**

***Shukrani***

***Utangulizi***

***SURA YA KWANZA***

***SEKTA YA AFYA KWA UJUMLA MKOANI RUVUMA***

*1. Miradi ya afya inayotekelezwa katika Mkoa wa Ruvuma*

*2.Shilingi bilioni saba zilivyoboresha sekta ya afya Ruvuma*

*3.Ujenzi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma*

*4.Tozo za simu zilivyojenga vituo vya afya kumi Ruvuma*

***SURA YA PILI***

***UJENZI WA HOSPITALI ZA WILAYA MKOANI RUVUMA***

*I. Uboreshaji miundombinu ya hospitali wilaya ya Nyasa*

*II.Ujenzi wa hospitali ya Halmashauri ya Mbinga wafikia asilimia 99*

*III.Waziri Mkuu aridhishwa na miundombinu hospitali ya Namtumbo*

*IV.Hospitali ya Madaba katika hatua za umaliziaji*

*V.Serikali yatoa milioni 500 kuanza ujenzi hospitali Manispaa ya Songea*

*VI.Milioni 500 zilivyoboresha miundombinu hospitali ya Mpitimbi*

*VI.Hospitali ya Namtumbo mkombozi wa wajaw*

## SURA YA TATU

## UJENZI WA VITUO VYA AFYA MKOANI RUVUMA

*A.Mradi wa kituo cha afya Liparamba wilayani Nyasa*
*B.Ujenzi wa kituo cha afya Mbangamao wilayani Mbinga*

*C.Mradi wa kituo cha afya Kingerikiti wilayani Nyasa*

*D.Menejimenti Ruvuma yakagua ujenzi kituo cha afya Liparamba*

*E. Menejimenti Ruvuma yakagua miradi ya afya Mbinga*

*F.Milango yote isiyokuwa na viwango Kingerikiti iondolewe-RC Ruvuma*

*H.Kituo cha afya Masonya Tunduru kuanza kutoa huduma*

*I.Mradi kituo cha afya Lilambo waanza kutoa huduma za afya*

*J.Mkoa wa Ruvuma ulivyodhamiria kukamilisha miradi ya afya*

*K.Songea wakamilisha ujenzi kituo cha afya Liganga*

*L.Mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Kindimbachini wilayani Mbinga*

*N.Mradi wa ujenzi kituo cha afya Subira Manispaa ya Songea*

*M.Mradi wa kituo cha afya Mkumbi wilayani Mbinga*

*O.Mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Magagura wilayani Songea*

*P.Mradi wa ujenzi kituo cha afya Mtakanini wilayani Namtumbo*

*Q.Mradi wa kituo cha afya Mchoteka wilayani Tunduru*

## *SURA YA NNE*

## *WODI ZA WAGONJWA WA DHARURA(EMD) MKOANI RUVUMA*

*I.Jengo la wagonjwa wa dharura hospitali ya Tunduru*

*II.Nyasa watakiwa kukamilisha jengo la EMD*

*III.Milini 630 zilivyokamilisha jengo la EMD hospitali ya Rufaa Songea*

*IV.Ufahamu mradi wa jengo la EMD katika hospitali ya Madaba*

## *SURA YA TANO*

## *UJENZI WA ZAHANATI KATIKA MKOA WA RUVUMA*

*A.Wananchi Mbinga waiomba serikali kukamilisha zahanati ya kijiji*

*B.Wananchi Kagugu Mbinga wakamilisha ujenzi wa zahanati*

*C.Wananchi Mbinga wataka zahanati yao ifunguliwe*

*D. Zahanati ya Kipingo Madaba ilivyosogeza huduma kwa wananchi*

## *SURA YA SITA*

## *MIRADI YA NYUMBA ZA WATUMISHI WA AFYA RUVUMA*

*1. Mradi wa nyumba moja ya familia tatu kituo cha afya Kalembo*

*2.Watumishi wa afya Kalembo waishukuru serikali*

*3.Mradi wa nyumba moja ya familia tatu kituo cha afya Kindimbachini*

*4.Mradi wa nyumba moja ya familia tatu kituo cha afya Kingerikiti*

## *SURA YA SABA*

## *VIFAATIBA KATIKA HOSPITALI MKOANI RUVUMA*

*A.Makabidhiano ya vifaatiba katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa*

*B.Wasimamizi uagizaji dawa Ruvuma wapata mafunzo*

*C.Mbunge Ruvuma atoa vifaa hospitali ya Tunduru*

*D.Hospitali ya KIUMA yapigwa jeki vifaatiba*

## *SURA YA NANE*

## *HABARI PICHA ZA MIRADI YA AFYA*

*1.Majengo ya hospitali ya wilaya ya Nyasa*

*2.Majengo kituo cha afya Lilambo Songea*

*3.Habari picha kituo cha afya Ligera Namtumbo*

*4.Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa yakagua mradi kituo cha afya Ligera*

*5.Mradi wa ujenzi wa hospitali ya Madaba*

*6.Mradi wa ujenzi wa hospitali ya Madaba*

*7.Waziri Mkuu akagua mradi wa hospitali ya Madaba*

*8.Muonekano wa mradi wa hospitali ya Madaba*

*9.Waziri ,Mkuu aweka jiwe la msingi hospitali ya Madaba*

*10.Mradi wa kituo cha afya Ligera Namtumbo*

## *SURA YA TISA*

## *HUDUMA NYINGINE ZA AFYA ZINAZOTOLEWA RUVUMA*

***I.****Huduma ya afya ya kinywa na meno*

***II.****Mkakati wa kutokomeza kifua kikuu Tunduru*

***III.****Mkoa wa Ruvuma ulivyodhamiria kupunguza udumavu*

*IV.Watu zaidi ya 63,000 Ruvuma wanaishi na virusi vya UKIMWI*

*V.Madaktari bingwa kutoka China walivyotoa huduma za kibingwa Songea*

*VI.Huduma ya afya ya mama na mtoto mkoani Ruvuma*

*VII.Huduma ya Lishe katika Mkoa wa Ruvuma*

## *SHUKRANI*

Kwa namna ya pekee namshukuru mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya njema hivyo kufanikisha kuandika Jarida la Ruvuma la Mkoa wa Ruvuma katika sekta ya ***afya mkoani Ruvuma ambalo linaangazia miradi ya hospitali,vituo vya afya, zahanati na huduma nyingine za kiafya ambazo zinatolewa na vituo vya kutolea huduma za afya katika mkoa wa Ruvuma.***

## UTANGULIZI

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya vituo 356 vinavyotoa huduma za afya. Kati ya vituo hivyo Hospitali ni 13 zikiwemo 6 za serikali, vituo vya afya 36 kati ya hivyo 10 ni vya mashirika ya dini, zahanati zipo 307 ambapo za serikali ni 246, Mashirika ya dini ni 26, zahanati tisa ni za mashirika ya umma na 26 ni za watu binafsi.

# SURA YA KWANZA

## SEKTA YA AFYA KATIKA MKOA WA RUVUMA

## 1.MIRADI YA AFYA INAYOTEKELEZWA KATIKA MKOA



***Pichani ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas***

Mkoa una jumla ya vituo **356** vinavyotoa huduma za afya. Kati ya vituo hivyo Hospitali ni **13** zikiwemo **6** za serikali, vituo vya afya **36** kati ya hivyo **10** ni vya mashirika ya dini, zahanati zipo **307** ambapo za serikali ni **246**, Mashirika ya dini ni **26, na 9** ni za mashirika ya umma na **26** ni za watu binafsi.

**a) Mapokezi ya Fedha za Utekelezaji wa Miradi ya maendeleo**

Kwa mwaka 2020/2021 Mkoa umepokea jumla ya **Shilingi 1,700,00.000.00** kwa ajili ya kujenga/kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya ambapo **Sh. 1,200,000,000.00** zilikuwa kwa ajili ya umaliziaji wa maboma **50** ya zahanati na Sh. **500,000,000.00** kwa ya kituo cha Afya Magazini.

Kwa mwaka 2021/2022 Mkoa umeendelea na ujenzi wa Hospitali tano (5) za Wilaya katika Halmashauri za Wilaya za Nyasa, Namtumbo, Madaba, Songea DC na Mbinga DC kwa gharama ya Tshs. **3,700,000,000.00.** Mkoa umepokea kiasi cha **Tshs. 7,250,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya **12** kupitia fedha za Tozo na Serikali Kuu**.** Pia Mkoa unaendelea na ujenzi wa vituo vya Afya vitatu **(3)** kupitia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri kwa gharama ya Tshs**. 1,500,000,000.00.** Kwa upande wa Zahanati Mkoa ulipokea kiasi cha Tshs. **1,050,000,000.00** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi wa Zahanati **21** kwenye Halmashauri saba (**7**).

Aidha, Mkoa umepokea pia kiasi cha shilingi **1,780,000,000.00** za kutekeleza Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19 - (**Mradi Na. 5144 TCRP)** kama ifuatavyo:

a) **Shilingi Milioni 630,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Watumishi wa sekta ya Afya kwa Halmashauri 7 (Madaba DC, Songea DC, Mbinga DC, Nyasa DC, Mbinga TC, Namtumbo DC & Tunduru DC)

b) **Shilingi Milioni 900** kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya dharura (emergency Medical Department-EMD) kwa Halmashauri za Madaba DC, Nyasa DC & Tunduru DC

c) **Shilingi 250,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa jengo la huduma za Wagonjwa mahututi (ICU) katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

d) **Taarifa ya Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa**

Mkoa ulipokea kiasi cha Tshs. **2,700,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa awamu ya kwanza ambao unahusisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la mionzi na nyumba ya mtumishi.

## 2.BILIONI SABA ZITAKAVYOBORESHA SEKTA YA AFYA RUVUMA




SERIKALI ya Awamu ya 6 inayoongozwa na Rais, Mhe. Dkt. Samia S. Hassan imetoa bilioni 7 kwa lengo la kuboresha utoaji huduma ya Afya kwa Wananchi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma

Akizungumza mbele ya Wataalamu kutoka Hospitali ya kanda ya Mbeya Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea. Dr, Magafu Majura amesema Hospitali imepokea Shilingi bilioni 7 kukamilisha mipamgo mikakati ya utoaji huduma kwa wananchi.

Dr. Majura amesema fedha hizo zimeelekezwa katika kujenga jengo la wagonjwa wa nje, jengo la huduma ya mionzi pamoja na nyumba moja ya mtumishi pia na ukarabati wa jengo la wangonjwa wenye uangalizi maalumu na jengo la dawa

Mbali na ujenzi na ukarabati huo ameeleza kuwa Serikali imeamua kuboresha utoaji huduma kwa Wananchi kwani imenunua vifaa tiba kimoja wapo ni *Mashine ya uchunguzi ya CT-Scan* ambayo itahudumia na kutoa matibabu kwa haraka na itasidia kuondoa msongamano wa wangonjwa

"Hii itatusaidia kwa wagongwa watakao hitaji kutibiwa katika Hospitali zetu za kanda na taifa kuweza kuanza kupata matibabu wakiwa bado wapo hapa kwamaana ya kuwasiliama kupitia tiba mtandao na madaktari wabobezi waliopo katika Hospitali zetu kubwa na kutupa majibu" Amesema Dr. Majura

Naye Mkurugenzi mtendaji wa Hospitali ya kanda ya Mbeya Dkt. Godlove Mwanji amesema Serikali imeamua kuboreha huduma za Afya ili wananchi wawe na uhakika wa kupata matibabu na kuepukana na gharama za kufuta matibabu kwenye hospitali kubwa za kitaifa

"Furaha yetu ni kwamba tumekuta miradi yoye hii imefikia hatua nzuri na siku si nyingi tutarajie kuwa itaanza kuwahudumia Wananchi tumeona vifaa vya kisasa vikitumika kutoa huduma jambo hili ni lakupongeza na kutoa shukrani kwa Serikali**"amesema Dkt.** Mwanji

Kwa upande wake Mkuu wa Idara ya magonjwa ya dharula na ajali Dr. Edson Francis ameeleza hali ilivyo sasa baada ya kukamilika kwa jengo hilo la wagonjwa wa dharula ambapo limesaidi kuhudumia wa wagonjwa wengi kwa haraka na kupata matibabu kwa muda mfupi

Hata hivyo Serikali imeboresha upatikanaji huduma mbalimbali katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma kwa nunua *mashine ya uchunguzi ya CT-Scan kwa mara ya kwanza ambayo itasaidia Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kutosafiri umbali mrefu Mbeya, Dodoma na Dar es salaamkwaajili ya vipimo.*

## 3.UJENZI WA HOSPTALI YA RUFAA YA MKOA WA RUVUMA




SERIKALI imetoa shilingi bilioni 3.4 kuendeleza ujenzi wa hospitali tano katika Mkoa wa Ruvuma.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas amezitaja hospitali ambazo ujenzi wake unaendelea kuwa ni ujenzi wa hospitali ya Rufaa ya

Mkoa ambapo katika awamu ya kwanza mradi unagharimu shilingi bilioni 2.7.

“Ujenzi katika hospitali ya Rufaa unahusisha jengo la wagonjwa wa nje OPD,jengo la mionzi na nyumba ya mtumishi”,alisema.

Amezitaja hospitali nyingine ambazo ujenzi wake unaendelea kuwa ni hospitali za Halmashauri za Nyasa,Mbinga,madaba na Songea.

Hata hivyo amesema hali ya upatikanaji wa dawa,vifaa tiba na vitendanishi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya mkoani Ruvuma imefikia asilimia 96.

RC Thomas amesema chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita Mkoa umejenga vituo vya afya 12 kupitia fedha za tozo na serikali kuu kwa gharama ya shilingi bilioni 7.8.

Ameongeza kuwa serikali pia imetoa zaidi ya shilingi milioni 856 kujenga nyumba tisa za watumishi wa afya na shilingi milioni 900 zimejenga majengo matatu ya Huduma za dharura (EMD) katika hospitali tatu za Tunduru,Nyasa na Madaba.

Baadhi ya wabunge akiwemo Mbunge wa Jimbo la Nyasa Mhandisi Stella Manyanya ameipongeza serikali kwa kuboresha miundombinu na vifaa katika hospitali ya Nyasa ambazo amesema zimesogeza huduma muhimu kwa wananchi.



## 4.TOZO ZILIVYOJENGA VITUO VYA AFYA KUMI RUVUMA



MKOA wa Ruvuma unaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 5.362 katika Halmashauri zote nane kupitia tozo ya miamala ya simu.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas amesema kati ya fedha hizo shilingi bilioni tano zimejenga vituo vya afya kumi na zaidi ya shilingi milioni 360 zimejenga vyumba vya madarasa 29.

Amesema miradi hiyo inatekelezwa katika Halmashauri zote nane mkoani Ruvuma ambapo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga miradi inayotekelezwa ina thamani ya zaidi ya shilingi bilioni moja.

Ameitaja miradi inayotekelezwa katika Halmashauri Mbinga kuwa ni ujenzi wa kituo cha afya Mkumbi na kituo cha afya Kindimbachini vinavyogharimu shilingi bilioni moja na umaliziaji wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari Nyoni na Litumbandyosi unaogharimu shilingi milioni 50.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa,Katika Halmashauri ya Madaba serikali imetoa kiasi cha shilingi milioni 525 kutekeleza miradi ya Kituo cha Afya Matetereka ambacho kinagharimu shilingi milioni 500 na ujenzi wa madarasa mawili katika sekondari ya Lipupuma ambayo yanagharimu shilingi milioni 25.

RC Thomas ameitaja miradi inayotekelezwa kupitia tozo ya miamala ya simu katika Halmashauri ya Mbinga Mji inagharimu shilingi milioni 537 ambazo zinatumika kutekeleza miradi ya ujenzi wa kituo cha Afya

Mbangamao ambacho kinatumia shilingi milioni 500 na umaliziaji wa vyumba viwili vya madarasa katika sekondari ya Kilimani na chumba kimoja sekondari ya Lamata ambavyo vinagharimu zaidi ya shilingi milioni 37.

Kanali Thmoas amesema katika Halmashauri ya Namtumbo serikali imetoa kiasi cha shilingi milioni 537 ambazo zinatumika kujenga kituo cha Afya Ligera ambacho kimetengewa shilingi milioni 500 na ukamilishaji wa vyumba viwili vya madarasa sekondari ya Nasuli na vyumba viwili sekondari ya Mbunga ambavyo vinatumia zaidi ya shilingi milioni 37.

Kulingana na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma,miradi inayotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa inagharimu shilingi milioni 537 ambapo shilingi milioni 500 zinatumika kujenga jengo la upasuaji,wodi ya akinamama katika kituo cha afya Liparamba,ujenzi wa nyumba ya watumishi wa afya,jengo la mionzi na njia ya kutembea wagonjwa.

Ameitaja miradi mingine inayotekelezwa katika Halmashauri ya Nyasa kuwa ni umaliziaji wa vyumba vya madarasa vitatu katika shule za sekondari Luhangarasi na Kingerikiti.

Mkuu wa Mkoa ameitaja miradi inayotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea kuwa ina thamani ya shilingi bilioni moja ambapo miradi inayotekelezwa ni ujenzi wa Kituo cha Afya Kilagano na kituo cha afya Liganga kila kimoja kikiwa na thamani ya shilingi milioni 500.

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea ameitaja miradi inayotekelezwa kupitia tozo ya miamala ya simu kuwa ina thamani ya shilingi milioni 550.

Ameitaja miradi hiyo kuwa ni Kituo cha Afya Subira kinachogharimu shilingi milioni 500 na ukamilishaji wa vyumba vinne vya madarasa katika shule za sekondari Lizabon,Luwawasi na Lukala vyenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 37.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma,miradi inayotekelezwa kupitia tozo ya miamala ya simu katika Halmashauri ya Tunduru inagharimu zaidi ya shilingi bilioni moja.

Hata hivyo amesema kati ya fedha hizo shilingi milioni 500 zinatekeleza ujenzi wa kituo cha afya Masonya na shilingi milioni 500 zinatekeleza mradi wa kituo cha afya Mchesi.

## SURA YA PILI

## UJENZI WA HOSPITALI ZA WILAYA MKOANI RUVUMA

### I. UBORESHAJI HOSPITALI YA WILAYA YA NYASA



SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi milioni 800 kujenga Hospitali ya wilaya Nyasa,ili kusogeza na kuboresha huduma za afya kwa wananchi ambao awali walilazimika kwenda nje ya wilaya hiyo kufuata matibabu.

Kaimu Mganga mfawidhi wa Hospitali ya wilaya Nyasa Dr Simon Yasin alisema,katika ujenzi huo baadhi ya majengo ikiwemo jengo la wagonjwa wa nje(OPD),wodi ya mama na mtoto na maabara yamekamilika na yameanza kutoa huduma.

Dr Yasin ametaja huduma zilizoanza kutolewa katika Hospitali hiyo ni za wagonjwa wa nje,huduma ya mama na mtoto,kulaza wagonjwa na upasuaji.

"kwa sasa tuko katika awamu ya tatu na ya mwisho kabisa ya utekelezaji wake,katika awamu hii tunajenga jengo la upasuaji kwa wanawake na wanaume,jengo la kuhifadhia maiti sambamba na jengo la dharura ambalo limegharimu shilingi milioni 300"alisema Dkt Yasin.

Kwa mujibu wa Dkt Yasin,majengo hayo yatakapokamilika yatasaidia wananchi wa wilaya hiyo kupata huduma bora za matibabu,kuokoa vifo vya akina wakati na baada ya kujifungua na kupunguza muda wa kwenda maeneo mengine kufuata huduma za afya.

Alisema,Hospitali hiyo ni kubwa na imejengwa eneo ambalo kila mmoja rahisi kufika na imesaidia sana wananchi wa Nyasa kupata huduma za afya karibu.

Dr. Yasini,amemshukuru Rais Dkt Samia Suluhu Hassan na serikali yake ya awamu ya sita, kwa kuridhia kutoa fedha zilizotumika katika utekelezaji wa mradi huo muhimu na mkubwa kwa ajili ya wananchi.

Aidha alisema kuwa,kujengwa kwa Hospitali hiyo na kuanza kutoa huduma za matibabu kumewapunguzia wananchi kero na usumbufu wa kutembea umbali mrefu hadi katika Hospitali nyingine kufuata matibabu.Ametoa wito kwa wananchi,kutumia zahanati,vituo vya afya na Hospitali zinazojengwa na serikali kwenda kupata huduma za matibabu kwa sababu zimejengwa kwa ajili yao.

Dr Yasin,amewashauri akina mama pindi wanapohisi dalili za ujauzito ni vyema wakawahi kliniki mapema ili kupata ushauri kwa ajili ya usalama wao na mtoto aliyeko tumboni na wakati na baada ya kujifungua.

Kwa upande wake Muuguzi wa Hospitali Lucia Lagila ametaja faida mojawapo kwa akina mama kuwahi kliniki ni kupunguza vifo vya mama na mtoto,kupata ushauri wa kitaalam wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua.

.

## II.UJENZI HOSPITALI YA MBINGA WAFIKIA ZAIDI YA ASILIMIA 99




MRADI wa ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya wilaya Mbinga mkoani Ruvuma unaotekelezwa kwa gharama ya Sh.bilioni 1.5 umefikia asilimia 99 ya utekelezaji wake.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo George Mhina amesema,hadi sasa majengo matano kati ya saba ambayo ni maabara,jengo la wangonjwa wa nje(OPD),kichomea taka,jengo la mionzi,jengo la bohari ya dawa na la kufuria yamekamilika.

“katika awamu ya tatu ambayo ni ya mwisho tutajenga jengo la wodi ya wazazi ambalo ndani yake kutakuwa na huduma ya upasuaji na kulaza akina mama wanaotoka kujifungua na jengo la utawala,tuko hatua ya mwisho ya kumpata mkandarasi atakayejenga jengo hilo”amesema Mhina.

Amesema,Hospitali hiyo itakapo kamilika itahudumia zaidi ya watu 255,000 kutoka vijiji vya Halmashauri ya Mbinga na wananchi wa wilaya jirani ya Songea na Nyasa.

Hali kadhalika amesema,kwa sasa wameanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje,hata hivyo matarajio yao katika kipindi cha miezi mitatu ijayo,waanze kutoa huduma ya upasuaji kwa akina mama wajawazito hasa wale watakaoshindwa kujifungua kwa njia ya kawaida.

Pia amesema,mwishoni mwa mwezi huu,wataanza kutoa huduma za mionzi( X-ray) na Ultrasound kwa kuwa jengo lake limekamilika na wanachosubiri kupata vifaa kutoka bohari ya dawa nchini(MSD)yenye dhamana ya kusambaza dawa na vifaa tiba kwenye vituo vya kutoa huduma za matibabu vya serikali.

Amemshukuru Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kutoa fedha ambazo zinatumika katika utekelezaji wa mradi huo na miradi mingine ya maendeleo kwa Halmashauri ya Mbinga.

Kwa upande wake Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo Amad Mwalukunga amesema,kuanza kwa huduma katika Hospitali hiyo kumewasaidia wananchi wa Halmashauri ya wilaya Mbinga kumaliza kero ya kwenda hadi Hospitali ya St Joseph Peramiho umbali wa kilomita 80 na Hospitali ya wilaya Mbinga iliyopo umbali wa km 20 kufuata matibabu.

Dkt Mwalukunga ametaja magonjwa yanayowasumbua wananchi wa ukanda wa Kigonsera ni malaria na hali hiyo inatokana na asilimia ni wakulima ambao wakati huu wa masika wengi wao wanaishi mashambani ambako wanakutana na changamoto ya kuumwa na mbu wanao sababisha ugonjwa huo.

Ameiomba Serikali kuitupia jicho Hospitali na kutoa fedha ambazo zitawezesha kukamilisha kabisa ujenzi wake ili wananchi waweze kupata huduma zote muhimu, badala ya kwenda maeneo mengine.

Mmoja wa wananchi aliyekutwa akipata matibabu Nassibu Mapunda,ameishukuru Halmashauri ya wilaya Mbinga kujenga Hospitali hiyo kwani licha ya kutokamilika,wameanza kupata huduma karibu na kupata muda kufanya kazi nyingine za kiuchumi.

Mapunda amesema,hapo awali walikuwa kwenye mateso makubwa ya kwenda Halmashauri nyingine kwa ajili ya kufuata matibabu, lakini sasa wanafurahi kuona baadhi ya huduma hizo zinapatikana karibu na makazi yao.

Hata hivyo,Mapunda ameiomba serikali kuwajengea barabara ya kutoka barabara kuu ya Songea-Mbinga hadi Hospitali kwa kiwango cha lami au changarawe ili kurahisisha usafiri wa kufika Hospitali.

## III.WAZIRI MKUU ARIDHISHWA NA MIUNDOMBINU HOSPITALI YA NAMTUMBO



WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema ameridhishwa na maboresho yaliyofanyika katika hospitali ya wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa Oktoba 18, 2022 alipofanya ziara hospitalini hapo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara katika hospitali hiyo na alieleza kutorishwa na milango iliyowekwa na kuagiza iondolewe na iwekwe mingine yenye viwango na leo Januari 06, 2023 amekagua maendeleo ya utekelezaji wa agizo na ameridhishwa na kazi iliyofanyika.

Kufuatia utekelezaji huo Waziri Mkuu amesema ameridhishwa na utekelezaji wa maelekezo hayo ambapo hadi sasa jumla ya milango 67 kati ya 84 imeondolewa na kuwekwa mipya yenye ubora.

“Leo nimeona milango bora kabisa, kwa nini tulikubali kuweka milango mibovu wakati mizuri ipo? Hii haikubaliki kwa sababu tunapoteza fedha za

Serikali zinazotokana na kodi ya wananchi. Ni lazima kila mtumishi wa umma atimize wajibu wake."

Amesema Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ya afya ili kusogeza huduma muhimu za kijamii karibu na wananchi.

Pia, Waziri Mkuu amewataka Wakuu wa Idara katika halmashauri zote nchini wasimamie kikamilifu utekelezaji wa shughuli zote za maendeleo katika maeneo yao ili kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa miradi zinatumika ipasavyo.




"Haipendezi kuona viongozi wakuu waje na kubaini madudu katika miradi wakati watendaji mpo. Kila mtumishi awajibike ipasavyo katika eneo lake ili kuhakikisha lengo la Mheshimiwa Rais Dkt. Samia la kuwaletea maendeleo wananchi linatimia."

Mradi wa ujenzi wa hospitali hiyo unatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 7.5, mpaka sasa hospitali hiyo imepokea shilingi bilioni 4.2 kutoka Serikali kuu ambapo majengo 20 yameshajengwa, majengo 13 yamekamilika, majengo saba yapo katika hatua za ukamilishaji. Hospitali itakapokamilika inatarajia kuhudumia watu Zaidi ya 200,000.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dkt. Festo Dugange amesema Serikali ya awamu ya sita itaendelea kuiboresha sekta ya afya ikiwemo kununua magari mawili kwenye halmashauri zote 184 nchini ikiwa moja nila wagonjwa na linguine ni kwa ajili ya usimamizi wa huduma za afya.

Akizungumza kuhusu ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana ya Namtumbo, Dkt. Dugange amesema watahakikisha wanasimamia maagizo yote yaliyotolewa na Waziri Mkuu ili kuhakikisha shule hiyo inakamilika kwa wakati na inaanza kudahili wanafunzi

Awali, Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo Dkt. Christopher Wabarumi aliishukuru Serikali kwa kuendelea kuboresha huduma za afya katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo na wilaya hiyo ambayo inaendelea na ujenzi wa majengo ya 22 katika hospitali ya wilaya hiyo.



Katikati ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas akitoa maagizo baada ya kukagua ujenzi wa hospitali ya Namtumbo

## IV.HOSPITALI YA MADABA KATIKA HATUA ZA UMALIZIAJI



SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi bilioni 2.9 hadi sasa kutekeleza mradi wa ujenzi wa hospitali ya Madaba Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.



UJENZI wa hospitali ya Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma upo katika hatua za umaliziaji.

Mkuu wa Wilaya ya Songea Mheshimiwa  amesema serikali imetoa shilingi bilioni 2.9 kutekeleza mradi huu ambao utawezesha kutoa huduma zote muhimu za matibabu.

Amesema hadi sasa zimetumika shilingi bilioni 2.2 kujenga majengo mbalimbali katika hospitali hiyo na kwamba serikali tayari imeleta shilingi milioni 700 ili kujenga wodi tatu ambazo ni za wanawake,watoto na wanaume pamoja na nyumba ya maiti.

“Wananchi walikuwa wanasafiri zaidi ya kilometa 120 kutoka Madaba hadi Songea kufuata huduma za matibabu katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa ,lakini sasa huduma zote muhimu zitatolewa hapa Madaba “,alisema Ndile.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Madaba Sajidu Idrisa Mohamed amesema tayari vifaa muhimu vya hospitali kama X-ray iliyogharimu shilingi milioni 350 imeshafungwa katika hospitali hiyo na kwamba kinachoendelea hivi sasa ni kufunga milango na kazi ndogo ndogo za ukamilishaji ili huduma za afya zianze kutolewa.

Halmashauri ya Madaba ni miongoni mwa Halmashauri tatu zinazounda Wilaya ya Songea.



## V.SERIKALI YATOA MILIONI 500 KUANZA UJENZI WA HOSPITALI MANISPAA YA SONGEA



Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imeanza kutekeleza Mradi wa ujenzi hospitali ya Manispaa ya Songea,mradi huo unatekelezwa katika Kata ya Tanga ambapo serikali imetoa shilingi milioni 500 kuanza kutekeleza mradi

## VI.SERIKALI YATOA MILIONI 500 KUBORESHA MIUNDOMBINU HOSPITALI YA MPITIMBI SONGEA




SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imetoa zaidi ya shilingi milioni 500 kujenga wodi mbili za upasuaji katika hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea iliyojengwa kwenye kijiji cha Mpitimbi Songea.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Neema Maghembe wakati anatoa taarifa ya mradi huo kwa Timu ya

Menejimenti Mkoa iliyoongozwa na Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma Ndugu Stephen Ndaki.

Maghembe amesema fedha hizo pia zimetumika kujenga nyumba ya mochwari na kichomea taka na kwamba serikali pia imetoa shilingi milioni 68 kupitia TASAF kujenga nyumba ya mtumishi wa hospitali hiyo.

Hadi sasa serikali imejenga majengo 13 kati ya 24 yanayotakiwa katika hospitali hiyo.



## VII.HOSPITALI YA NAMTUMBO UKOMBOZI WA WAJAWAZITO



SERIKALI imekamilisha ujenzi wa majengo nane ya hospitali ya wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma ambapo kazi iliyokuwa imebaki ya kuunganisha mfumo wa umeme na maji safi imekamilika.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo Dr.Godwin Luta anasema Halmashauri hiyo,imekamilisha ujenzi wa hospitali ya wilaya ambao umetokana na jitihada za serikali ya awamu ya Tano za kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma ya matibabu jirani na maeneo wanayoishi.

Serikali inayoongozwa na Rais Dkt.John Magufuli imedhamiria kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi na kuwekwa msisitizo kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 ambapo hadi sasa vimejengwa vituo vya afya na hospitali katika maeneo mbalimbali nchini.

“Ujenzi huu umefanyika kwa awamu tano ambapo kwa mwaka 2010/2011,Halmashauri yetu ilipokea fedha kutoka serikali kuu kiasi cha

shilingi milioni 450 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala na wagonjwa wa nje'',anasema Dr. Luta.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo Venance Nachimbinya anabainisha zaidi kuwa kati ya fedha zilizotolewa,katika jengo la wodi ya wazazi zimetumika zaidi ya shilingi milioni 176 na jengo la wodi ya wanaume zimetumika zaidi ya shilingi milioni 259.

Anabainisha zaidi kuwa jengo la upasuaji limegharimu zaidi ya shilingi milioni 213,jengo la stoo ya dawa zaidi ya shilingi milioni 203,jengo la maabara milioni 164,jengo la kufulia zaidi ya milioni 113,jengo la mionzi zaidi ya milioni 136,jengo la wodi ya wanawake zaidi ya milioni 166 na jengo la watoto zaidi ya milioni10.

Christina Mndeme ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma anawaagiza watendaji wa Halmashauri ya Namtumbo kuhakikisha majengo yaliyokamilika yanaanza kutumika kutoa huduma kwa wananchi wa Namtumbo ili kutimiza azma ya serikali ya kusogeza huduma ya afya karibu na wananchi.

"Wananchi hawataki kuona majengo. Badala yake wanataka kupata huduma za afya katika hospitali ,serikali imetekeleza wajibu wake wa kutoa fedha za kukamilkisha ujenzi '',anasisitiza Mkuu wa Mkoa.

John Milazi Mkazi wa Namabengo anasema kutekelezwa kwa mradi huo kunamfanya ajisikie amani kwa sababu akinamama na watoto kwa miaka mingi walikuwa wanapata shida.



## SURA YA TATU

## UJENZI WA VITUO VYA AFYA MKOANI RUVUMA

### A.KITUO CHA AFYA LIPARAMBA NYASA



Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma Ndugu Stephen Ndaki akiwa na Timu ya Menejimenti Mkoa wamekagua mradi wa ujenzi kituo cha afya Liparamba Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa unaotekelezwa kwa shilingi milioni 500.

## B.MRADI  WA KITUO CHA AFYA MBANGAMAO MBINGA



SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi milioni 500 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kituo cha afya Mbangamao Halmashauri ya Mji wa Mbinga

## C.KITUO CHA AFYA KINGEREKITI KUANZA KUTOA HUDUMA



MRADI wa ujenzi wa kituo cha Afya Kingerekiti Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma ambacho serikali imetoa shilingi milioni 500 upo katika hatua za Mwisho za ukamilishaji ili kianze kutoa huduma kwa wananchi.

## D.MENEJIMENTI MKOA WA RUVUMA YAAGIZA UJENZI KITUO CHA AFYA LIPARAMBA UKAMILIKE



MENEJIMENTI Mkoa wa Ruvuma ikiongozwa na Katibu Tawala wa Mkoa Ndugu Stephen Ndaki imeuagiza uongozi wa Halmashauri ya Willaya ya Nyasa kusimamia kikamlifu ujenzi wa kituo cha afya Liparamba ambao serikali imetoa shilingi milioni 500 uweze kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Akizungumza baada ya ukaguzi wa mradi huo Ndaki amesema serikali imetoa fedha za kutekeleza mradi huo muda mrefu ambapo hadi sasa bado mradi haujakamillika kwa asilimia 100 hivyo ameaagiza kasi ya kukamilisha mradi iongezwe huku akisisitiza mradi ukamillike kwa ubora na viwango vinavyolingana na thamani ya fedha.

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan imetoa kwa nyakati tofauti jumla ya shilingi milioni 500 kujenga majengo ya kituo hicho ambapo katika awamu ya kwanza zilitolewa shilingi milioni 250 kujenga jengo la upasuaji na wodi ya wazazi na katika awamu

ya pili zimetolewa milioni 250 kujenga jengo la wagonjwa wa nje OPD na jengo la maabara .

## E.MENEJIMENTI MKOA WA RUVUMA YAKAGUA MIRADI YA AFYA YA MILIONI 900 MBINGA



Menejimenti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI Mkoa wa Ruvuma ikiongozwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Ndugu Stephen Ndaki imekagua miradi minne ya afya katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga yenye thamani ya shilingi milioni 900.

Miradi iliyokaguliwa ni ujenzi wa kituo cha afya Mbangamao wenye thamani ya shilingi milioni 500,kituo cha afya Miyangayanga chenye thamani ya shilingi milioni 250,mradi wa nyumba ya mtumishi ya familia tatu katika kituo cha afya Kalembo iliyogharimu shilingi milioni 90 na zahanati ya Kijiji cha Matarawe iliyogharimu shilingi milioni 67.

Akizungumza baada ya kukagua miradi hiyo Ndaki ameipongeza Halmashauri ya Mji wa Mbinga kwa kusimamia miradi hiyo,hata hivyo ameagiza dosari zilizojitokeza katika hatua za umaliziaji hasa kwenye milango zifanyiwe marekebisho.Katibu Tawala huyo ameagiza kasi ya kukamilisha miradi kwa wakati na kwamba miradi yote ikamilike kwa asilimia 100 ili ianze kutoa huduma kwa wananchi.



Mradi wa jengo la upasuaji katika kituo cha Afya Mbangamao Halmashauri ya Mji wa Mbinga

## F.MILANGO YOTE ISIYOKUWA NA VIWANGO KITUO CHA AFYA KINGERITI NYASA IONDOLEWE-RC RUVUMA



MKUU wa mkoa wa Ruvuma Kanal Laban Thomas,ameagiza kuondolewa milango yote iliyofungwa katika Hospitali ya wilaya Nyasa na kituo cha Afya Kingerikiti wilayani humo,baada ya kubaini mbao zilizotumika kutengenezea kutokuwa na ubora unaotakiwa.

Kanal Laban ametoa agizo hilo kwa nyakati tofauti,baada ya kukagua ujenzi wa kituo cha Afya Kingerikiti ambacho serikali imetoa zaidi ya shilingi milioni 390 kutekeleza mradi huo ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 95 na ujenzi wa wodi tatu katika Hospitali ya wilaya ya Nyasa ambapo serikali imetoa shilingi milioni 800 kutekeleza mradi huo.

Laban,ametoa onyo kali kwa mafundi wanaojenga miradi mbalimbali ya maendeleo na kusisitiza kuwa,mkoa huo sio wa kujifunzia bali ni mkoa unaohitaji mafundi wenye uwezo na wanaofanya kazi kwa weledi ili miradi inayotekelezwa ilingane na thamani halisi ya fedha zinazotolewa.

“haiwezekani hata kidogo fundi amekwenda kuokota mabanzi na kuja kutufungia kwenye jengo letu,jambo hili sikubaliani nalo hata kidogo,nakuagiza hakikisha unafanya marekebisho ya milango yote haraka tena kwa gharama zako”alisema.

Alisema,kamwe hawezi kukubaliana na mambo ya ovyo yanayofanywa na baadhi ya watendaji wa umma wanaoshindwa kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo yenye lengo la kusukuma kasi ya kukua kwa uchumi wa mkoa huo na kuwataka watumishi wa Halmashauri ya Nya kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Alisema Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan,imepeleka zaidi ya Sh.bilioni 1 katika wilaya hiyo kwa ajili ya kujenga vituo viwili vya afya vya Lipalamba na Kingerikiti ili kuimarisha huduma za afya kwa wananchi,hivyo hakuna sababu ya wananchi wa maeneo hayo kuendelea kukosa huduma.

Aidha Laban, ametoa wiki mbili kwa viongozi wa wilaya ya Nyasa, kuhakikisha wanamaliza ujenzi wa kituo cha Afya Kingerikiti ili wananchi waanze kupata huduma za matibabu.

“hiki kituo kilipaswa kukamilika tangu mwaka jana,lakini naona hadi leo hii ujenzi wake bado haujakamilika,sasa natoa wiki mbili mfanye marekebisho na kianze kutoa huduma”alisema Kanal Laban.

Akiwa katika Hospitali ya wilaya,Kanal Laban amesikitishwa kukuta milango yote inayoendelea kufungwa katika majengo ya kutolea huduma ikiwa imepishana na baadhi mbao zake zikiwa mbichi.

Mkuu wa mkoa wa Ruvuma,ameagiza fundi aliyetengeneza milango hiyo kutolipwa fedha hadi atakapofanya marekebisho kwa kuwa amekwenda kinyume na mkataba.

Majengo yanayojengwa ni mochwari,jengo la upasuaji kwa wanawake na wanaume na njia za watembea kwa miguu mradi unaotekelezwa kwa gharama ya Sh.milioni 800 ikiwa ni uendelezaji wa awamu ya tatu ya ujenzi wa Hospitali hiyo.

Kwa upande wake Mkuu wa wilaya hiyo Filbetho Sanga,amehaidi kufanyia kazi maagizo ya Mkuu wa mkoa na mapungufu yote yaliyobainika katika ujenzi wa miradi hiyo hasa milango.

Dc Sanga,amewataka wakandarasi wanaofanya kazi katika wilaya hiyo kuhakikisha kazi wanazofanya zinakuwa bora na hatopokea mradi wowote uliojengwa chini ya kiwango.

Mkazi wa kijiji cha Kingerikiti Zakari Mbele,ameiomba serikali kukamilisha haraka ujenzi wa kituo cha afya Kingerikiti ili waanze kupata huduma za matibabu karibu na makazi yao.

**G.MBINGA WAJENGA KITUO CHA AFYA MATIRI**



HALMASHAURI ya wilaya Mbinga mkoani Ruvuma,imetumia Sh.milioni 500 kutoka mapato ya ndani kujenga kituo cha afya Matiri kata ya Matiri ikiwa ni utekelezaji wa mkakati wake wa kusogeza na kuimarisha huduma za afya kwa jamii.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo George Mhina amesema,fedha hizo zimetumika kwa ajili ya kujenga majengo matano ambayo ni jengo la wagonjwa wa nje(OPD)maabara,jengo la wazazi, jengo la kufulia na kichomea taka ambalo ujenzi wake utaanza hivi karibuni.

Amesema,ujenzi wa majengo hayo umekamilika kwa asilimia zaidi ya 90 na Halmashauri imepanga kuanza kutoa huduma angalau za awali mapema mwezi April.

Mhina amesema,kwa sasa kazi inayofanyika ni kutambua watumishi watakaokwenda kufanya kazi katika kituo hicho,kuleta madawa na vifaa tiba pamoja na usajili wake.

Amesema,Halmashauri ya wilaya Mbinga kupitia mapato yake ya ndani imejipanga kuhakikisha vijiji na kata zote kuna vituo vya kisasa vya kutolea huduma ili wananchi ambao ndiyo wanufaika wanafurahia na kwenda kwenye vituo vya serikali kupata huduma mbalimbali za matibabu.

**H.KITUO CHA AFYA MASONYA TUNDURU KUANZA KUTOA HUDUMA**



Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Masonya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma ambacho serikali imetoa shilingi milioni 550 hadi sasa kutekeleza mradi huo.Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Ruvuma ikiongozwa na Mwenyekiti wake Komred Odo Mwisho imetembelea na kukagua mradi huo

## I.KITUO CHA AFYA LILAMBO CHAANZA KUTOA HUDUMA




Kiruo cha Afya Kata ya Lilambo Manispaa ya Songea ambacho kimejengwa na serikali kupitia mapato ya ndani kwa gharama ya shilingi milioni 514 kimeanza kutoa huduma kwa wananchi.

Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Ruvuma ikiongozwa na Mwenyekiti wake Komred Odo Mwisho imekagua mradi huo na kupongeza baada ya kuanza kutoa huduma za matibabu kwa wananchi.

## J.MKOA WA RUVUMA ULIVYODHAMIRIA KUKAMILISHA UJENZI WA VITUO VYA AFYA



MKUU wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas ameuagiza uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya Lilambo na Mletele ili vianze kuwahudumia wananchi.

Kanali Thomas ametoa maagizo hayo baada ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Halmashauri hiyo.

Amesema kumekuwa na changamoto ya umaliziaji wa miradi hivyo ameuagiza uongozi wa Manispaa ya Songea kutoa fedha za kumalizia vituo vya afya.

Amesema serikali inaendelea kutoa mabilioni ya fedha kutekeleza miradi mbalimbali ambapo Serikali kupitia mapato ya ndani katika Manispaa ya Songea imetoa shilingi milioni 514 kutekeleza ujenzi Kituo cha Afya Lilambo na zaidi ya shilingi milioni 545 zimetolewa na serikali Kuu kupitia Global Fund kutekeleza ujenzi kituo cha afya Mletele.

“Nichukue fursa hii kuwapongeza Manispaa ya Songea kwa kusimamia ujenzi wa kituo cha Afya Lilambo ambacho kinatumia mapato ya ndani ,hata hivyo ongezeni kasi ili mkamilishe ujenzi wa Kituo hiki ulioanza mwaka jana “,alisisitiza RC Thomas.

Mkuu wa Mkoa pia amekagua ujenzi wa madarasa 14 kati ya 76 yanayojengwa katika shule za sekondari Manispaa ya Songea kwa gharama ya shilingi bilioni 1.5.

Ameagiza ujenzi wa madarasa hayo na samani zake kukamilika kama ilivyopangwa kwa kuzingatia viwango ili yaanze kutumika Januari 2023.

Amewaagiza wakuu wa Wilaya kujenga utamaduni wa kukagua mara kwa mara miradi yote ya maendeleo ambayo serikali inatoa fedha.

Akitoa taarifa ya miradi hiyo kwa Mkuu wa Mkoa,Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Dkt.Federick Sagamiko amesema katika kipindi cha Julai 2021 hadi Oktoba 2022,Manispaa hiyo imepokea shilingi bilioni 2.7 toka serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta za elimu,afya,Utawala na Maendeleo ya Jamii.

Mkuu wa Wilaya ya Songea Mheshimiwa Pololet Mgema amesema licha ya changamoto zilizopo ujenzi wa madarasa 96 katika Wilaya hiyo unaendelea vizuri na wanatarajia kumkabidhi madarasa hayo Mkuu wa Mkoa Desemba 10 mwaka huu.

Amewaagiza waandisi wanaosimamia miradi kuwa kwenye miradi wakati wote ili itekelezwe kwa viwango.Ameahidi dosari zote zilizojitongeza kwenye ukaguzi kufanyiwa kazi haraka.

Wilaya ya Songea inaundwa na Halmashauri tatu za Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Halmashauri ya Madaba na Halmashauri ya Wilaya ya Songea.



## K.SONGEA WAKAMILISHA UJENZI WA KITUO CHA AFYA LIGANGA



WANANCHI wa vijiji vitatu vya kata ya Liganga na vijiji vingine vinavyopakana na kata hiyo katika Halmashauri ya wilaya Songea,wanatarajiwa kuondokana na changamoto ya upatikanaji wa huduma ya afya waliyokuwa wanakabiliana nayo kwa muda mrefu, kufuatia ujenzi wa kituo cha afya kinachojengwa katika kata hiyo kukamilika kwa

asilimia 98.

Mkuu wa idara ya afya,ustawi wa jamii na lishe wa Halmashauri hiyo Dkt Geofrey Kihaule alisema,kituo hicho kinajengwa katika kijiji cha Selekano ambapo kwa gharama ya Sh.milioni 500 ambazo zimetolewa na Serikali kwa awamu mbili.

Dkt Kihaule alisema,katika awamu ya kwanza serikali ilitoa kiasi cha Sh.milioni 250 ambazo zilitumika kujenga jengo la wagonjwa wa nje(OPD)maabara,na kichomoea taka ambapo majengo hayo yamekamilika kwa asilimia 100.

Alisema,majengo hayo yanatarajiwa kufunguliwa katika kipindi cha mwezi mmoja ujao na kuanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa magonjwa ya nje wanaofika kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali za matibabu.

Kwa mujibu wa Dkt Kihaule,watumishi watatu watakao fanya kazi katika kituo hicho wameshafika na kwa sasa wapo katika zahanati ndogo ya misheni ya Liganga wakisaidia kutoa huduma kwa wananchi huku wakisubiri kufunguliwa kwa kituo hicho.

Aidha alisema,katika awamu ya pili Halmashauri imepokea jumla ya Sh.milioni 250 kwa ajili ya kujenga majengo pacha ambayo ni ya huduma ya mama na mtoto,upasuaji pamoja na jengo la kufulia ambayo yote kwa sasa yamekamilika.

Dkt Kihaule,ameiomba serikali kuwasaidia kupata vifaa vikiwamo vya maabara mapema ili waweze kuanza kutoa huduma, kwani majengo yote yamekamilika na kinachosubiri ni kupata vifaa vya upasuaji,maabara na vitanda kwa ajili ya kulaza wagonjwa.

Alisema,kituo hicho kinatarajiwa kuwahudumia watu wengi zaidi kuliko kituo chochote cha afya katika Halmshauri ya wilaya Songea wakiwamo wafanyakazi zaidi ya elfu nne wa shamba la kahawa la kampuni ya Aviv Ltd ambao wengi wanaishi katika kijiji cha Liganga.

Dkt Kihaule alitaja wanufaika wengine ni wananchi wa kijiji cha Liganga,Seekano,wafungwa na askari wa gereza la Kitai,wafanyakazi wa migodi ya makaa ya mawe,wananchi wa kijiji cha Amanimakoro kilichopo wilaya jirani ya Mbinga, wananchi wa kijiji cha Mbinga Mhalule,Matomondo na Lipokela.

Alisema,kukamilika kwa kituo hicho ni ufumbuzi mkubwa sio kwa wananchi wa kata ya Liganga tu, bali hata kwa watu wengine wanaotumia barabara ya Songea-Mbinga ambao wakipata ajali na shida nyingine watakimbilia katika kituo hicho kwa ajili ya kupata msaada wa matibabu.

Mwenyekiti wa kijiji cha Selekano Magreth Haule,ameishukuru serikali kupitia Halmashauri hiyo kuwajengea kituo cha afya kwani awali walilazimika kutembea umbali mrefu na kutumia gharama kubwa Kwenda kupata matibabu maeneo ya mbali.

Amempongeza Mbunge wa JImbo la Peramiho na Waziri wa nchi ofisi ya Rais menejimenti ya utumishi wa umma na utawala bora Jenista Mhagama,kwa kazi nzuri anayofanya ya kuwahudumia wananchi wa jimbo hilo na kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya Songea Neema Maghembe alisema,tayari wamepokea jumla ya watumishi 39 wa kada mbalimbali katika sekta ya afya ambao wamesharipoti na wanaendelea kufanya kazi ya kuwahudumia wananchi.

Maghembe alisema,katika kipindi cha mwaka mmoja wamepokea Sh.bilioni 1 zinazotokana na tozo kwa ajili ya kujenga vituo viwili vya afya katika kata ya Liganga na Mgazini.

Aidha alieleza kuwa, wamepokea fedha nyingine kiasi cha Sh.milioni 500 kwa ajili ya kujenga jengo la upasuaji na majengo mengine katika Hospitali ya Halmashauri iliyopo kijiji cha Mpitimbi ambayo imeshaanza kutoa huduma kwa wananchi wa Songea na wale wanaotoka nchi jirni ya Msumbiji.

Maghembe alisema, katika mkakati wa kusogeza huduma kwa wananchi wamefanikiwa kujenga zahanati katika kijiji cha Ndongosi kwa gharama ya Sh.milioni 50 na zahanati nyingine katika kijiji cha Makwaya kata ya Lilahi ambapo wananchi walilazimika Kwenda maeneo mengine kufuata matibabu.

Pia alisema, wamepokea kiasi Sh.milioni 104 ambazo zitatumika kuboresha mazingira ya kujifungulia kwa akina mama wajawazito katika zahanati mbalimbali ambapo kwa sasa wananchi wa maeneo hayo wanaendelea kufurahia huduma bora za afya.

Maghembe amewaasa wananchi kutumia zahanati,vituo vya afya na Hospitali zinazojengwa kwenda kupata huduma bora za afya kwani serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili yao na kuachana na mira zilizopitwa na wakati zinazodai ukiwa mtu wa kwanza kupata huduma kwenye vituo na Hospitali zinazojengwa unaweza kupoteza maisha.

## L.UJENZI KITUO CHA AFYA KINDIMBACHINI MBINGA



SERIKALI inajenga Kituo cha Afya Kindimbachini Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma.Mradi huo unatekelezwa kwa shilingi milioni 500 kupitia tozo za miamala ya simu.

Serikali kwenye mradi huo pia imejenga nyumba moja ya watumishi yenye uwezo wa kuchukua familia tatu hali ambayo itawawezesha madaktari na wauguzi wanaofanya kazi kwenye kituo hicho kuwa jirani na kituo cha kazi hivyo kuwahudumia wagonjwa kwa ufanisi

## N.MRADI WA KITUO CHA AFYA SUBIRA MANISPAA YA SONGEA



SERIKALI imetoa shilingi milioni 500 kutekeleza ujenzi wa Kituo cha Afya Subira Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma kupitia fedha za tozo ya miamala ya simu .

Kwa miaka mingi wananchi wa Kata ya Subira walikuwa wanasafiri umbali mrefu kufuata huduma za matibabu katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa mjini Songea.

## M. MRADI WA KITUO CHA AFYA MKUMBI WILAYA YA MBINGA



SERIKALI imetoa shilingi milioni 500 kutekeleza ujenzi wa Kituo cha Afya Mkumbi Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma kupitia fedha za tozo ya miamala ya simu

## O.KITUO CHA AFYA MAGAGURA WILAYA YA SONGEA



SERIKALI imetoa jumla ya shilingi milioni 400 kutekeleza mradi wa kituo cha afya Magagura kilichojengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.Kukamilika kwa kituo hicho kunasogeza huduma za afya kwa wananchi wa Magagura,Chipole na maeneo jirani.

Serikali kwa muda mfupi imeweza kujenga vituo vya afya Magagura,Liganga,Muhukuru na Kilagano katika Halmashauri ya wilaya ya Songea hivyo kusogeza huduma za afya jirani na wananchi ambao kwa miaka mingi walikuwa wanaangaika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za matibabu.

## P.MRADI WA KITUO CHA AFYA MTAKANINI NAMTUMBO



SERIKALI imetoa zaidi ya shilngi milioni 400 kutekeleza mradi wa kituo cha afya Mtakanini Halmashauri ya wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma.Kukamilika kwa mradi huu kumesogeza huduma ya afya jirani ya wananchi hivyo kupunguza kero ya wananchi kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma ya matibabu .

Kituo cha afya Mtakanini kimemaliza kero ya muda mrefu ya wananchi wa Kijiji hicho kusafiri hadi mjini Songea kufuata huduma za matibabu katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma

**Q.MRADI KITUO CHA AFYA MCHOTEKA WILAYA YA TUNDURU**




SERIKALI imetumia shilingi milioni 400 kuboresha kituo cha afya Mchoteka kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma.Uboreshaji huo umeboresha pia huduma mbalimbali za afya zinazotolewa katika kituo hicho ikiwemo huduma za upasuaji.



## SURA YA NNE

## MRADI WA WODI ZA DHARURA MKOANI RUVUMA

### 1.JENGO LA WAGONJWA WA DHARURA EMD TUNDURU LAKAMILIKA



Mradi wa ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura katika hospitali ya Wilaya ya Tunduru lililogharimu shilingi milioni 300 umekamilika na serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan tayari imenunua vifaa vya kisasa ambavyo vimefungwa katika hospitali ya wilaya ya Tunduru tayari kwa kuanza kutoa huduma za dharura kwa



## 2.HOSPITALI YA NYASA WATAKIWA KUKAMILISHA JENGO LA WAGONJWA WA DHARURA EMD



KATIBU Tawala Mkoa wa Ruvuma Ndugu Stephen Ndaki akiwa na Timu ya Menejimenti Mkoa wamekagua mradi wa ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa Dharura (EMD) katika hospitali ya wilaya ya Nyasa ambalo serikali imetoa shilingi milioni 300 kutekeleza mradi huo ambao hadi sasa bado haujakamilika kwa asilimia 100 .

Akizungumza baada ya ukaguzi wa jengo hilo Ndaki amesikitishwa na ucheleweshaji wa mradi huo ambapo amesema kuna changamoto kubwa kwenye umaliziaji wa fremu na ufungaji milango na kwamba kazi ya kuanza kufunga vifaa kwenye jengo la EMD imechelewa ukilinganisha na hospitali nyingine za Tunduru na Madaba ambazo tayari zimefunga vifaa kwenye kwenye majengo hayo.

Amesema kasi ya umaliziaji ni ndogo hivyo ameuagiza uongozi wa Halmashauri hiyo kuongeza kasi ya ukamilishaji na kufanya marekebisho kwenye frame na milango ambapo amewataka kusimamia utekelezaji wa miradi kuanza hatua za awali hadi mwisho ili utekelezaji wake uwe wenye viwango na ubora.

Kwa upande wake Mkuu wa WIlaya ya Nyasa Mheshimiwa Filibetho Sanga amesema kumekuwa na usimamizi mbovu kwenye miradi ya serikali hali inayosababisha miradi kutekelezwa chini ya viwango na miradi mingine kutokamilika kwa wakati

## 3.MILIONI 630 ZAKAMILISHA JENGO LA WAGONJWA WA DHARURA HOSPITALI YA RUFAA RUVUMA




HIZI ni juhudi za Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Rai Dkt.Samia Suluhu Hassan katika uboreshaji na utapikanaji wa matibabu kwa Wananchi kwa kujenga Jengo la wagonjwa wa dharura katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea lililogharimu shilingi milioni 630

**4.MRADI WA JENGO LA WAGONJWA WA DHARURA EMD KATIKA HOSPITALI YA MADABA**



Mradi wa ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura katika hospitali ya Halmashauri ya Madaba wilayani Songea lililogharimu shilingi milioni 300,mradi umekamilika na serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan tayari imenununua vifaa vya kisasa ambavyo vimefungwa katika hospitali ya wilaya hiyo tayari kwa kuanza kutoa huduma za dharura



## SURA YA TANO

## UJENZI WA ZAHANATI KATIKA MKOA WA RUVUMA

### I.WANANCHI MBINGA WAIOMBA SERIKALI KUKAMLISHA UJENZI WA ZAHANATI YA KIJIJI



BAADHI ya Wananchi wa mtaa wa Kipika kata ya Matarawe Halmashauri ya mji Mbinga mkoani Ruvuma,wameiomba serikali kukamilisha haraka ujenzi wa zahanati yao ili waweze kuondokana na adha wanayoipata ya kufuata matibabu mbali na makazi yao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wamesema, kwa sasa ujenzi wa zahanati hiyo umesimama kutokana na kukosekana kwa fedha, hivyo wameiomba serikali kutafuta mbinu mbadala ambazo zitawezesha kukamilika kwa ujenzi huo.

Amina Pili amesema,kwa muda muda mrefu wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma za afya na wakati mwingine akina mama wajawazito wanajifungulia njiani wakati wakifuata huduma na kuingia gharama kubwa ya usafiri hasa nyakati za usiku.

Amesema,wananchi wa mtaa huo kwa kiasi kikubwa wanategemea kupata huduma katika Hospitali ya wilaya Mbuyula pekee iliyopo umbali wa km 5 na hakuna njia mbadala,jambo linalo sababisha baadhi yao kushindwa kuwahi katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa wakati na hivyo kupoteza maisha yao.

Mwenyekiti wa serikali ya mtaa wa KipikaThomas Mahundi,ameipongeza Halmashauri ya mji Mbinga kuona umuhimu wa kupeleka ujenzi wa zahanati hiyo ambayo itamaliza kero na usumbufu kwa wananchi wa mtaa wa Kipika na kata ya Matarawe kwenda maeneo mengine kufuata huduma za afya.

Amesema,zahanati hiyo itakapokamilika itawezesha na kusaidia kupunguza foleni ya wagonjwa katika Hospitali ya wilaya Mbinga,na kuiomba serikali kufanya haraka kukamilisha zahanati hiyo ambayo itakuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi.

Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya mji Mbinga Dkt Maximo Magehema amesema, ujenzi wa zahanati hiyo umefikia asilimia 98 na gharama za ujenzi wake ni Sh.milioni 93 kati ya hizo shilingi milioni 62 zimeshatumika.

Dkt Magehema amesema,zahanati hiyo itakapokamilika itasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya mji Mbinga na kusaidia kusogeza huduma za afya kwa wananchi wa kata ya Matarawe.

Ameeleza kuwa,zahanati hiyo itawezesha wananchi kupata huduma karibu na makazi yao na watoto wadogo kupata huduma muhimu za chanjo,badala ya wazazi wao kulazimika kwenda mbali kwa ajili ya huduma hizo.

Aidha,amewataka wananchi wa kata hiyo kupenda kushiriki na kuchangia nguvu zao katika shughuli mbalimbali za maendeleo,badala ya kuichia serikali peke yake kwani kufanya hivyo itasaidia miradi inayoibuliwa na kutekelezwa kukamilika kwa wakati.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji Mbinga Grace Quintine amesema,kwa mwaka wa fedha 2022/2023 wamepokea kiasi cha shilingi milioni 150 kutoka serikali kuu zilizotumika kujenga zahanati tatu ikiwamo ya kata ya Matarawe ambayo ujenzi wako uko hatua ya mwisho kukamilika.

Quintine amesema,zahanati hiyo na nyingine zitakapomilika zitasaidia kutatua changamoto ya wananchi wa maeneo husika kutembea umbali mrefu na kutumia muda mwingi kwenda maeneo mengine kufuata huduma za afya.

Aidha amesema, Halmashauri ya Mji Mbinga kutoka mapato ya ndani imetenga na kutumia shilingi milioni 89 zilizofanikisha kujenga zahanati mbili ambazo zimekamilika na kuanza kutoa huduma za afya kwa wananchi.

## II.WANANCHI KAGUGU MBINGA WAKAMILISHA UJENZI WA ZAHANATI




WAKAZI wa kijiji cha Makatani kata ya Kagugu Halmashauri ya Mji Mbinga mkoani Ruvuma,wanatarajia kuondokana na adha ya kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 25 kila siku kwenda kata jirani ya Tingi kufuata huduma za afya.

Wakazi hao wamepata matumani mapya baada ofisi ya Mkurugenzi wa mji Mbinga kuingilia kati na kuanza kukamilisha ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho iliyoanza kujengwa zaidi ya miaka 17 bila kukamilika.

Diwani wa kata ya Kagugu Batson Mpogolo amesema, zahanati hiyo ilianza kujengwa mwaka 2006 kwa nguvu za wananchi lakini ujenzi wake ulisimama kutokana na kukosa fedha za kukamilisha ili huduma ziweze kutolewa.

Mpogolo ameishukuru Halmashauri ya Mji Mbinga kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha kazi ya ujenzi wa zahanati hiyo ambayo imekamilika kwa asilimia 95.

Kwa mujibu wa Mpogolo, kazi zilizobaki katika ujenzi huo ni kuchimba matundo ya vyoo na kujenga kichomea taka na kuwaomba wananchi wa kata hiyo kuendelea kuvuta subira wakati huu ambao serikali iko hatua za mwisho kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo.

Hata hivyo,ameiomba serikali kuharakisha kwa kuleta vifaa tiba na wahudumu ili zahanati iweze kuhudumia wananchi ambao bado wanaendelea kuteseka kwa kwenda maeneo mengine kufuata huduma za afya.

Mtendaji kata wa Kagugu John Makoyole amesema,kata ya Kagugu yenye zaidi ya wakazi 1,820 kuna zahanati moja tu ya Makatani ambayo bado haijaanza kufanya kazi,hivyo wananchi wanalazimika kwenda kata nyingine kufuata huduma.

Amesema,hali hiyo imesababisha wananchi wengi kuwa maskini kwa kuwa wanakosa muda wa kufanya kazi za maendeleo,badala yake wanatumia muda mwingi kwenda maeneo mengine kufuata huduma za afya.Ameishuru serikali kwa uamuzi wake wa kumalizia kazi ya ujenzi wa zahanati hiyo ili wananchi wapate huduma za afya karibu na maeneo.

Aidha,ameipongeza serikali ya awamu ya sita kwa kuendelea kuboresha baadhi ya huduma za kijamii ikiwamo maji,barabara na nishati ya umeme ambapo kati ya vijiji vitano vya kata hiyo,vitatu vimefikiwa na umeme.

Eliza Mapunda mkazi wa kijiji hicho amesema,kukamilika kwa zahanati kutawezesha kuanza kutumika na kupunguza gharama walizokuwa wakitumia kusafiri kwenda mbali kufuata huduma za afya zinazopatikana kata za jirani na Hospitali ya wilaya Mbinga mjini.

Amesema,kwa sasa wanalazimika kutumia gharama kubwa kati ya shilingi 10,000 hadi 15,000 kwa usafiri wa boda boda kwenda kata ya Tingi kupata matibabu jambo lililowatesa kwa muda mrefu.

Mkazi mwingine Mathias Sangana amesema, kukamilika kwa zahanati hiyo italeta hamasa kubwa kwa akina mama wajawazito kuanza kliniki mapema na kujifungulia Hospitali kuliko sasa ambapo wajawazito wengi wanachelewa kuhudhuria kliniki mapema kutokana na gharama kubwa ya usafiri.

Kwa upande wake mwakilishi wa Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji Mbinga Dkt Maximo Magehema amesema,serikali kupitia Halmashauri yam ji Mbinga iko hatua ya mwisho kukamilisha ujenzi wake.

## III.WANANCHI MBINGA WATAKA ZAHANATI IFUNGULIWE



. BAADHI ya wananchi wa kata ya Luwaita Halmashauri ya mji Mbinga wilayani Mbinga,wameiomba serikali kupitia Halmashauri ya Mji Mbinga,kukamilisha ujenzi wa zahanati ya Luwaita kutokana na ujenzi wake kuchukua zaidi ya miaka 5 bila kukamilika.

Wamesema kukosekana kwa huduma za afya katika kata hiyo,kumesababisha akina mama wajawazito kulazimika kujifungulia njiani kutokana na vituo vya afya vilivyopo kuwa umbali wa zaidi ya kilomita 7 kutoka katika maeneo wanayoishi.

Wameiomba Halmashauri ya mji Mbinga ,kuwahurumia kutokana na mateso wanayopata kutumia muda mwingi kwenda kupata huduma maeneo mengine kwa kuanza mchakato wa kufungua na kutoa baadhi ya huduma katika zahanati hiyo ambayo sehemu kubwa ujenzi wake umekamilika.

Bosco Komba amesema, zahanati hiyo ilianza kujengwa kwa muda mrefu kwa wananchi kuchangia nguvu zao ili waweze kupata huduma za matibabu karibu,hata hivyo wanashangazwa na ukimya wa serikali

kushindwa kufungua na kutoa huduma kwa wananchi.

Maria Nchimbi amesema,wananchi wa kata ya Luwaita wanatamani kuona zahanati hiyo ikianza kutoa huduma kwani wamechoka kuvumilia kutembea umbali mrefu kila wanapohitji kupata huduma za matibabu ambazo zinapatikana kwenye vituo vilivyopo mbali na makazi yao.

Mtendaji wa kijiji cha Luwaita Rehema Ameir ameeleza kuwa,awali mpango wa serikali ulikuwa kituo cha afya,lakini kukosekana kwa nguvu kazi za wananchi ikaamua iwe zahanati kwa kuwa zilihitajika nguvu za pamoja kati ya serikali na wananchi wa eneo husika.

Hata hivyo amesema,ujenzi wa zahanati ya Luwaita umekamilika kwa asilimia 99 na wakazi zaidi ya 4,000 wanatarajia kupata huduma mara itakapoanza kutoa huduma,lakini kuchelewa kufunguliwa kunatokana na kukosekana kwa vyoo na kichomea taka.

Amesema,zahanati hiyo itarahisisha upatikanaji wa huduma na kuwaondolea wananchi adha ya kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta huduma kwenye vituo vingine vya afya na kupunguza muda mwingi wanaopaswa kujikita katika shughuli za maendeleo.

Kwa upande wake kaimu mganga mkuu wa Halmashauri ya mji Mbinga Dkt Maximo Magehema amesema,kimsingi zahanati hiyo imekamilika na serikali ipo katika hatua ya mwisho kuanza kutoa huduma na kuwaomba wananchi kuwa wavumilivu wakati serikali ikikamilisha mambo muhimu ya kiutendaji ikiwamo vifaa na watumishi.

Amesema,serikali ya awamu ya sita kupitia Halmashauri ya mji Mbinga imejipanga kuhakikisha kila kijiji kina zahanati na kata kituo cha afya ili kusogeza na kuboresha huduma za afya kwa wananchi wake.

## IV.ZAHANATI YA KIPINGO MADABA ILIVYOSOGEZA HUDUMA JIRANI NA WANANCHI




Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Ruvuma ikiongozwa na Mwenyekiti wake Komred Odo Mwisho imetembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa zahanati ya Kipingo Kata ya Lituta Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma ambapo serikali imetoa shilingi milioni 100 kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo ambayo tayari imeanza kutoa huduma kwa wananchi

# SURA YA SITA

## MIRADI YA NYUMBA ZA WATUMISHI WA AFYA

### A.MRADI WA NYUMBA MOJA YA FAMILIA TATU KITUO CHA AFYA KALEMBO MBINGA



Mradi wa ujenzi wa nyumba ya mtumishi yenye uwezo wa kuchukua familia tatu katika kituo cha afya Kalembo Halmashauri ya Mji wa Mbinga ambayo serikali imetoa shilingi milioni 90 kutekeleza mradi huo ambao tayari umekamilika



## B.WATUMISHI WA AFYA KITUO CHA AFYA KALEMBO WAISHUKURU SERIKALI KWA NYUMBA



WATUMISHI wa kituo cha Afya Kalembo Halmashauri ya Mji Mbinga,wameishukuru serikali kwa kuwajengea nyumba bora za kuishi na kueleza kwamba zimewaongezea morali ya kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi wanaofika kupata matibabu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti watumishi hao wamesema,nyumba hizo zimewafanya kuipenda kazi yao kwa sababu zimewaondolea msongo wa mawazo na changamoto ya mahali pa kuishi,tofauti na awali walipokuwa wamepanga nyumba mitaani ambazo hazikuwa na sifa ya kuishi mtumishi wa umma.

John Mtinda amesema,kutokana na mazingira ya ardhi la eneo hilo kuwa na tope jingi hasa nyakati za masika, ilikuwa vigumu kwao kufika kwa wakati inapotokea dharura ya kuhitajika kazini kuhudumia wagonjwa baada ya muda wa wakati kutokana na ubovu wa barabara kutoka kwenye makazi yao hadi kazini.

Amesema, kujengwa kwa nyumba hizo ni faraja kubwa kwao kwani zimesaidia sana kupata mahali pazuri na uhakika pa kuishi na kuhaidi

kuzitunza nyumba hizo na kuongeza morali ya utendaji wa majukumu yao ya kila siku.

Ameipongeza serikali ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kupitia Halmashauri ya Mji Mbinga,kujenga nyumba hizo karibu na eneo la kazi na kueleza kuwa,zimemaliza kabisa changamoto ya mahali pa kuishi kwa watumishi wa kituo hicho.

Mariam William mtaalam wa maabara amesema, kabla ya nyumba hizo walikuwa wanateseka kuhudumia wagonjwa hasa nyakati za usiku kutokana na kuishi mbali na eneo la kazi,lakini sasa wanapata muda wa kutosha na wanafika kwa wakati hata inapotokea dharura ya kuhitajika kazini.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji Mbinga Maximo Magehema amesema,mpango wa Halmashauri ya Mji Mbinga ni kuhakikisha kila kinapojengwa kituo cha afya kunakuwa na nyumba ili kuwawezesha watumishi kuishi jirani na eneo la kazi ili waweze kutoa huduma kwa wakati.

Amesema,mpango huo ni endelevu kwa sababu utasaidia watumishi wa afya wanaoletwa na kufanya kazi katika Halmashauri ya mji Mbinga kuwa na mazingira mazuri,kuipenda kazi yao na kutojutia kuwepo katika Halmashauri hiyo.

Amewataka wananchi,kuendelea kutumia zahanati,vituo vya afya na Hospitali zilizopo na zinazoendelea kujengwa kwenda kupata huduma za matibabu kwa sababu serikali inajenga miradi hiyo kwa lengo la kusogeza na kuboresha huduma kwa wananchi.

## C.MRADI WA NYUMBA MOJA YA FAMILIA TATU KITUO CHA AFYA KINDIMBACHINI



Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi milioni 90 kujenga nyumba moja ya familia tatu katika kituo cha afya Kindimbachini Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma



**D.MRADI WA NYUMBA MOJA YA FAMILIA TATU KATIKA KITUO CHA AFYA KINGERIKITI NYASA**



Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi milioni 90 kujenga nyumba moja ya familia tatu katika kituo cha afya Kingerikiti Halmashauri ya wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma



## SURA YA SABA:

## VIFAATIBA KATIKA HOSPITALI ZA MKOA WA RUVUMA

### I.MAKABIDHIANO YA VIFAATIBA MTANDAO KATIKA HOSPITALI YA RUFAA SONGEA



**Wagonjwa kupata huduma za kibingwa ndani ya Mkoa**

SERIKALI kupitia Wizara ya Afya imekabidhi vifaa vya tiba mtandao katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma hali ambayo itawawezesha wananchi kupata huduma bobezi za kibingwa ndani ya Mkoa.

Akizungumza mara baada ya kukabidhi vifaa hivyo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma,Mwakilishi wa Wizara ya Afya ambaye pia ni Mratibu wa Tiba Mtandao,Dr. Ligile Vumilia amesema huduma hiyo ni muhimu hasa kwa wananchi wanaoishi pembezeni kama Mkoa wa Ruvuma.

Amesema wananchi wote ambao watakuwa wanahitaji huduma za afya za kibingwa na bobezi sasa watazipata katika hospitali ya Rufaa ya Ruvuma badala ya kusafiri umbali mrefu ambapo serikali

imeichagua hospitali hiyo kuwa ni miongoni mwa hospitali tano za mwanzo kabisa nchini kupatiwa huduma hiyo.

Dr.Vumilia amesema kuletwa kwa vifaa hivyo katika hospitali ya Rufaa Mkoa wa Ruvuma ni kutekeleza maagizo ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alipofanya uzinduzi wa X-Ray katika hospitali ya Mkoa wa Ruvuma mwaka 2019,aliagiza kuanzisha huduma ya tiba mtandao katika hospitali hiyo.

“Serikali kupitia Wizara ya Afya imeichagua Hospitali za Rufaa za Ruvuma,Bombo Tanga, Mkoa wa Katavi na hospitali mbili za Wilaya za Nzega na Chato kuwa hospitali za mwanzo kufungiwa huduma ya tiba mtandao”,alisisitiza Dr.Vumilia.

Amesema Mfuko wa Mawasiliano kwa wote umetoa shilingi bilioni moja kwa ajili ya kununua vifaa tiba mtandao kwa ajili ya hospitali tano nchini na kwamba vifaa vya tiba mtandao vinapelekwa katika hospitali hizo na vitaunganishwa kwajili ya kuanza kazi ya kutoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa.

Hata hivyo amesema Taasisi ya Teknolojia nchini inatarajia kufunga vifaa vya tiba mtandao baada ya makabidhiano hayo ambapo katika hospitali ya Rufaa ya Ruvuma chumba maalum kimeshaandaliwa kwa ajili ya kufungwa vifaa hivyo.

Kwa mujibu wa Mratibu huyo,huduma hiyo inatarajiwa kutolewa katika hospitali za Rufaa 21 nchini na kwamba huduma ya tiba mtandao katika hospitali hizo itaunganishwa na hospitali za Kanda za Bugando Mwanza,Kanda ya Benjamin Mkapa Dodoma na Kanda ya Mbeya.

“Tutakuwa na hospitali nne za kitaifa ambazo zitakuwa na huduma bobezi za kibingwa ambazo ni hospitali ya Taifa Muhimbili,hospitali ya mishipa na mifupa ya fahamu ya MOI,hospitali ya saratani ya Ocean Road na Taasisi ya Jakaya Kikwete ambayo ni maalum kwa magonjwa ya moyo”,alisisitiza Dr.Vumilia.

Amesema huduma ya tiba mtandao katika hospitali ya Rufaa ya Ruvuma itamwezesha mgonjwa yeyote kupata huduma bobezi za

kibingwa bila kusafiri umbali mrefu kama hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma Dr.Magafu Majura amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa msaada wa vifaa vya tiba mtandao ambao utawawezesha wananchi kufanyiwa vipimo mkoani Ruvuma na vipimo hivyo kutumwa kwa njia ya mtandao hivyo mgonjwa kufahamu ugonjwa wake akiwa Ruvuma hivyo kupunguza gharama za usafiri na malazi kwa mgonjwa.

"Kwa kutumia vifaa vya tiba mtandao tutakuwa sawa na waliopo Dar es salaam,wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na nchi jirani za Msumbiji na Malawi sasa watapata huduma za kibingwa wakiwa Songea",alisisitiza Dr.Majura.

Naye Afisa Mawasiliano wa Wizara ya Afya Catherine Sungura amesema serikali pia imetoa shilingi milioni 630 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma na kwamba katika nchi nzima serikali inajenga majengo ya wagonjwa wa dharura katika hospitali nane za rufaa.

Sungura amesema pia serikali imetoa shilingi milioni 150 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU) katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma ambapo miradi yote hiyo imetekelezwa kwa asilimia 100.

.

## II.WASIMAMIZI UAGIZAJI WA DAWA RUVUMA WAPATA MAFUNZO



Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI imeendesha mafunzo ya siku tatu ya kuwajengea uelewa wasimamizi ngazi ya Mkoa wa Ruvuma na Halmashauri zote nane wanaohusika na mfumo wa uagizaji dawa,vifaatiba na vitendanishi.

Mafunzo hayo ambayo yamefanyika katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma mjini Songea yamefunguliwa na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Jeremiah Sendoro.

Mafunzo yamelenga kuwaelimisha wasimamizi ngazi ya Mkoa na Halmashauri kuhusu mwongozo wa mfumo wa mshitili ambao ulianzishwa rasmi mwaka 2018 na Wizara ya Afya lengo likiwa ni kuhakikisha wadau wote wanafuata mwongozo wa mshitili kwenye uagizaji dawa,vitendanishi na vifaa tiba.



Baadhi ya washiriki mafunzo ya uagizaji dawa kutoka Halmashauri zote nane zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma wakipata mafunzo ya siku tano ya kuagizaji dawa,vifaatiba na vitendanishi



Moja ya majengo katika mradi wa ujenzi wa hospitali ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma

## III.MBUNGE ATOA VIFAA TIBA KATIKA HOSPITALI YA TUNDURU



MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Ruvuma(CCM) Mheshimiwa Mariam Nyoka,ametoa msaada wa vifaa tiba mbalimbali katika Hospitali ya wilaya Tunduru mkoani humo ikiwa ni kutimiza azima yake ya kupunguza baadhi ya changamoto zilizopo katika Hospitali hiyo na kusaidia upatikanaji wa huduma bora za afya.

Vifaa vilivyotolewa ni mashuka 30 na chandarua 15 kwa ajili ya wodi ya akina mama,mashine za kupimia magonjwa yasioambukiza(BP na Sukari) kwa wananchi watakaofika kupata huduma ya matibabu katika Hospitali hiyo.

Akizungumza baada ya kukabidhi vifaa hivyo Nyoka alisema, msaada huo unatokana na dhamira yake ya muda mrefu kabla hajawa Mbunge kwa kutoa kile alichonacho kuisaidia jamii yenye shida na kuunga mkono jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali kuhakikisha nchi yetu inakuwa na watu wenye afya bora.

Alisema,kipaumbele chake cha kwanza kama Mbunge wa vitu maalum ni kusaidia katika sekta ya afya kwa kuwa sekta hiyo ni moja ya nguzo kuu na yenye mchango mkubwa katika kuleta mabadiliko ili kuwa na watu wenye afya njema, wenye uwezo wa kufanya kazi za kujiletea maendeleo yao na kushiriki kukuza uchumi wa mkoa wa Ruvuma nchi yetu.

Nyoka,amewakumbusha watoa huduma katika Hospitali hiyo na sekta yote ya afya mkoani Ruvuma,kutoa huduma bora kwa wananchi bila kubagua kwani ni sehemu muhimu na wajibu wao.

Kwa upande wake Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo Dkt Athuman Mkonohumo, amemshukuru Mbunge huyo kwa kutoa vifaa tiba ambavyo vitakwenda kuboresha huduma za afya na kuongeza juhudi za serikali za kuboresha huduma za afya katika Hospitali hiyo.

Dkt Athuman alisema,vifaa hivyo vitawasaidia watumishi kutekeleza vyema majukumu yao ya kila siku na wananchi kupata huduma bora za matibabu.

Pia,ametoa wito kwa mashirika,taasisi ,wadau na viongozi wengine wenye uwezo,kujitokeza na kuisaidia Hospitali kwani bado inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwamo upungufu wa vitanda na vifaa vingine kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma za afya.

Muuguzi Mfawidhi wa Hospitali hiyo Nelly Simon amesema,vifaa hivyo vinakwenda kusaidia na kuboresha suala zima la matibabu katika Hospitali hiyo ambayo inakabiliwa na idadi kubwa ya wagonjwa.




Mbunge wa viti Maalum Wanawake Mkoa wa Ruvuma Mheshimiwa Mariam Nyoka akikabidhi mashuka kwa uongozi wa hospitali ya wilaya ya Tunduru

## IV.HOSPITALI YA KIUMA TUNDURU YAPIGWA JEKI VIFAATIBA



HOSPITALI ya Kiuma inayomilikiwa na Kanisa la Upendo wa Kristo Masihi wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma,imepokea msaada wa mashine ya X-Ray kwa ajili ya wagonjwa wanaohitaji kufanyiwa uchunguzi magonjwa mbalimbali ikiwamo ya mionzi.

Mashine hiyo imetolewa na shirika la Neno na Tendo(Word&Deed)kutoka nchini Ujerumani ambayo ni ya kwanza kwa ukubwa na ubora,katika Hospitali binafsi na Serikali kwa ukanda wa mikoa ya kusini.

Hayo yamesemwa na Mganga Mkuu wa Hospitali hiyo Dkt Nzelipa Masaga,wakati akitoa taarifa kwa Mkuu wa wilaya hiyo Julius Mtatiro aliyeambatana na Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini Hassan Kungu na mwakilishi wa shirika la Word&Deed Susanna Diechmann.

Alisema,uhusiano uliopo kati ya Kanisa la Upendo wa Kristo Masihi na Shirika hilo ndiyo uliowezesha kupatikana kwa mashine hiyo ya kisasa(Digital) ambayo imeanza kuwa msaada mkubwa watu wanaofika kupata huduma ya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali.

DKT Nzelipa Masaga alisema,mashine hiyo ina uwezo wa kupima na kutambua kwa haraka magonjwa na shida nyingine katika mwilini tofauti na mashine iliyokuwepo zamani(Manual). Alisema, X-ray mpya ni suluhisho kubwa kwa watu wanaotoka maeneo mbalimbali hasa ikizingatia kuwa, Halmashauri ya wilaya ya Tunduru imeipa Hospitali hiyo jukumu la kusimamia jumla ya zahanati tisa za vijiji jirani na kituo cha afya kimoja.

Alisema kuwa,kupatikana kwa mashine hiyo ni ukombozi mkubwa kwa wagonjwa wanaofika kupata matibabu na wanaotakiwa kufanyiwa uchunguzi kwa njia ya mionzi.

Kwa mujibu wa Dkt Masaga,mashine hiyo ina uwezo wa kubaini matatizo ya wagonjwa wengi kwa wakati mmoja itasaidia kumaliza msongamano wa kusubiri vipimo kwa muda mrefu kwa watu wanaofika katika Hospitali.

Dkt Masaga alisema, kupatikana kwa mashine hiyo kunaashirikia mwanzo wa katika uboreshaji wa huduma za afya zinazotolewa na Kanisa hilo kwa kushirikiana na wadau shirika la Word&Deed kwani sasa wamefanikiwa hata kupanua huduma za matibabu ikiwamo ya mivunjiko(wanaopata ajali).

Dkt Masaga alifafanua kuwa,siku za nyuma walishindwa kutoa huduma ya uchunguzi kwa wagonjwa wengi kwa kuwa X-ray iliyokuwepo haikuwa na uwezo wa kutambua matatizo kwa haraka,hivyo baadhi ya wagonjwa walilazimika kwenda hadi Hospitali ya wilaya Tunduru mjini umbali wa km 67 kufuata huduma ya X-ray.

Hata hivyo alisema, changamoto kubwa ni upungufu mkubwa wa watumishi kwani mahitaji 105 na waliopo ni 56,na kuiomba serikali kutafuta njia ya kuwasaidia watumishi ambao wataongeza nguvu ya kuhudumia wananchi wanaofika katika Hospitali ya Kiuma.

Kwa upande wake mwakilishi wa shirika la Word&Deed Susanna Diechmanna amehaidi kuwa, shirika hilo litaendelea kusaidia vifaa mbalimbali kwa Hospitali hiyo ili iweze kuboresha na kutoa huduma bor

Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini Hassan Kungu ameripongeza shirika la Word&Deed kwa msaada huo, kwa sababu wananchi wa Jimbo la Tunduru kaskazini na mkoa wa Ruvuma wana uhakika wa kupata huduma ya mionzi karibu na haraka.

Mkuu wa wilaya ya Tunduru Julius Mtatiro,licha ya kuwashukuru wafadhili hao kwa misaada mbalimbali wanayotoa kwa Kanisa la Upendo,amewataka wafanyakazi wa Hospitali hiyo kuhakikisha wanatunza vifaa hivyo ili viweze kudumu kwa muda mrefu

## SURA YA NANE

## HABARI PICHA ZA MIRADI YA AFYA MKOANI RUVUMA

### 1.BAADHI YA MAJENGO HOSPITALI YA NYASA



Baadhi ya majengo katika mradi wa ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma.

**2.BAADHI YA MAJENGO KITUO CHA AFYA LILAMBO SONGEA**







Baadhi ya majengo katika kituo cha afya Lilambo Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma

### 3.HABARI PICHA KITUO CHA AFYA LIGERA NAMTUMBO



Katikati ni Mwenyekiti wa Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Ruvuma Komred Odo Mwisho akitoa maelekezo kwa Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Ligera Namtumbo ambacho serikali imetoa shilingi milioni 500 kujenga Kituo hicho

**4.KAMATI YA SIASA YA CCM MKOA YAAGIZA JENGO LA WAZAZI KITUO CHA AFYA LIGERA LIVUNJWE**




Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Ruvuma imeagiza jengo la wodi ya wazazi katika kituo cha Afya Kata ya Ligera Halmashauri ya Namtumbo livunjwe kutokana na ujenzi wake kuwa chini ya kiwango.Mwenyekiti wa Kamati hiyo Komred Oddo Mwisho akizungumza baada ya kutembelea na kukagua mradi wa Kituo

cha Afya Ligera unaogharimu shilingi 500,Komred Mwisho amesema Kamati haijaridhishwa na ujenzi wa wodi hiyo  na mradi mzima ambao umechelewa kukamilika .

## 5.MRADI WA UJENZI HOSPITALI YA MADABA SONGEA



SERIKALI imetoa shilingi bilioni 2.9 kutekeleza ujenzi wa hospitali ya Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.

## 6.MRADI WA UJENZI HOSPITALI YA MADABA



Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni mbili hadi sasa kutekeleza mradi wa hospitali ya Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma

## 7.WAZIRI MKUU AKAGUA UJENZI WA HOSPITALI YA MADABA SONGEA



Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa amekubali kuweka jiwe la msingi kwenye mradi wa ujenzi wa hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan hadi sasa imetoa zaidi ya shilingi bilioni mbili kutekeleza mradi huo.

Waziri Mkuu alikuwa mkoani Ruvuma katika ziara ya siku mbili ya kikazi ambayo ameifanya katika Halmashauri za Namtumbo na Madaba.

## 8.MUONEKANO WA HOSPITALI YA MADABA KWA JUU



Muonekano wa majengo ya hospitali ya Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea Mkoani Ruvuma ambayo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alikagua Ujenzi wake na kuweka jiwe la Msingi la ujenzi huo mkoani Ruvuma, Oktoba 19, 2022



Moja ya majengo katika mradi wa ujenzi wa hospitali ya Madaba wilaya ya Songea mkoani Ruvuma,mradi wa hospitali upo mbioni kuanza kutoa huduma za matibabu kwa wananchi

## 9.WAZIRI MKUU AKIWEKA JIWE LA MSINGI MRADI WA HOSPITALI YA MADABA



Waziri Mkuu wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa akiweka jiwe la msingi mradi wa ujenzi wa hospitali ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma



## 10 MRADI WA UJENZI WA HOSPITALI YA MADABA



Baadhi ya majengo katika mradi wa hospitali ya Madaba wilaya ya Songea mkoani Ruvuma ambapo serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 2.7 hadi sasa kutekeleza mradi huo

## 11.MRADI WA KITUO CHA AFYA KATA YA LIGERA NAMTUMBO



SERIKALI imetoa shilingi milioni 500 kujenga Kituo cha Afya Kata ya Ligera Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma.Fedha hizo zimetokana na tozo za miamala ya simu.

## SURA YA TISA:

## HUDUMA NYINGINE ZA AFYA ZINAZOTOLEWA MKOANI RUVUMA

### A.HUDUMA YA AFYA YA KINYWA NA MENO



***Pichani ni Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dr.Louis Chomboko***

Mkoa wa Ruvuma unatarajia kufanya wiki ya afya ya kinywa na meno kuanzia Machi 14,2023 hadi Machi 20,2023.

Kulingana na taarifa ya Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa Ruvuma,kila Halmashauri itaadhimisha wiki hiyo kwa kutoa elimu ya kinywa na meno kwa jamii .

Katika wiki hiyo pia utafanyika uchunguzi wa kinywa na meno kwa wanafunzi wa shule za msingi wanaosoma madarasa ya Awali,darasa la kwanza hadi la tatu.

Maadhimisho ya afya ya kinywa na meno kitaifa mwaka huu yalifanyika mkoani Kigoma.

## B.MKAKATI WA KUTOKOMEZA KIFUA KIKUU TUNDURU




HOSPITALI ya wilaya Tunduru mkoani Ruvuma,kupitia kitengo cha kifua kikuu na ukoma imefanikiwa kuibua jumla ya wagonjwa 1,028 sawa na asilimia 122.2 kati ya lengo la kuibua wagonjwa 841 hadi kufikia mwezi Disemba mwaka 2022.

Hayo yamesemwa na Mganga Mkuu wa wilaya hiyo Dkt Wilfred Rwechugura,wakati akitoa taarifa ya kampeni dhidi ya mapambano ya ugonjwa wa kifua kikuu inayofanyika katika vijiji mbalimbali wilayani humo kwa mwaka 2023.

Dkt Rwechungura alisema,kati ya hao wagonjwa 70 sawa na asilimia 6.8 walikutwa na maambukizi ya VVU ambapo watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na tano waliokutwa na vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu ni 245 sawa na asilimia 23.8.

Kwa mujibu wa Dkt Rwechungura,watoto chini ya miaka mitano wanaoishi na wagonjwa wa kifua kikuu waliochunguzwa na kupimwa 196 na

walioanza dawa kinga185,wanaoishi na wagonjwa wa TB na wakabainika kupatwa na ugonjwa huo ni 17 na waliofariki dunia 17 sawa na asilimia 1.6.

“kimsingi ugonjwa wa kifua kikuu katika wilaya yetu bado ni tatizo kubwa,hata hivyo tunaendelea na mapambano kupitia kampeni zinazofanyika katika maeneo mbalimbali,lengo letu ni kutokemeza kabisa ugonjwa huo”alisema.

Alisema,tatizo la ugonjwa wa kifua kikuu katika wilaya hiyo linatokana na uwepo wa machimbo ya madini ambayo yana mkusanyiko wa watu wengi, hivyo ni rahisi kuambukizana pamoja na ukosefu wa nyumba bora hasa maeneo ya vijijin.

Dkt Rwechungura, ameitaka jamii kujenga nyumba bora zenye uwezo wa kuingiza hewa ya kutosha na wale watakaona dalili za ugonjwa huo ni vyema kuwahi katika vituo vya kutolea huduma kwa ajili ya uchunguzi badala ya kukaa nyumbani au kukimbilia kwa waganga wa tiba asili.

Alieleza kuwa,katika kipindi hicho watu waliogundulika na ugonjwa wa ukoma ni 85 waliopima VVU ni 85 sawa na asilimia 100 na hakuna aliyebainika kupata virusi vya ukimwi.

Aidha alisema, katika kipindi hicho watu wanaoishi na wagonjwa wa Ukoma na wakachunguzwa walikuwa 52,ambapo hakuna aliyegundulika kuwa na ugonjwa huo na wagonjwa wa ukoma waliopata viatu ni 29 na wagonjwa 37 wana ulemavu wa kudumu.

Amewashukuru wadau wanaotoa huduma za afua mbalimbali za afya zikiwamo za kifua kikuu,ukimwi na ukoma ambao wamekuwa washiriki wazuri katika kuhakikisha afya za wananchi wa wilaya hiyo zinaimarika.

Kwa upande wake Mratibu wa kifua kikuu na ukoma wa wilaya hiyo Dkt Mkasange Kihongole alisema,kwa mwaka 2023 serikali kupitia wizara ya afya imewapa malengo ya kuibua wagonjwa 874.

Alisema,Halmashauri ya wilaya Tunduru kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kupitia mkakati wa kudhibiti kifua kikuu na ukoma itahakikisha dawa za kutibu kifua kikuu zinapatikana wakati wote na zinatolewa bila malipo na kuimarisha uwezo wa vituo vya ugunduzi wa TB.

Alitaja mikakati itakayofanikisha kuwapata wagonjwa hao ni kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu ugonjwa huo unavyoenea,dalili na namna ya kujikinga na maeneo yatakayohusika ni shule za msingi na sekondari za kutwa na bweni.

Mkasange alitaja mkakati mwingine ni kuhakikisha familia zote zinazoishi na wagonjwa wa TB zinafanyiwa uchunguzi na wale watakaobainika wataanzishiwa matibabu yanayotolewa bila malipo(bure)kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za matibabu.

Alisema, katika kampeni hizo watashirikiana na wahudumu wa afya ngazi ya jamii wanaofanya kazi ya kusanya sampuli za makohozi na kuzipeleka Hospitali kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi kwa kutumia mashine za kupimia sampuli za makohozi yaani Gene-Xpert.

Amewataja wadau wengine watakaoshirikiana nao kwenye mapambano ya kifua kikuu ni pamoja na shirika lisilo la Kiserikali la MDH na vyombo vya Habari ambavyo vina mchango na nafasi kubwa ya kupeleka elimu ya ugonjwa huo kwa jamii.

Dkt Mkasange,amewaonya waganga wa tiba asili na tiba mbadala,kuacha tabia ya kuwakumbatia wateja wenye dalili za kifua kikuu ili kuepuka uwezekano wa kuambukizwa wao wenyewe na wateja wanaofika kwenye vilinge vyao.

Mkazi wa mtaa wa Nakayaya Yusufu Juma anayeugua ugonjwa wa kifua kikuu,amewashukuru wataalam wa kitengo cha kifua kikuu katika Hospitali ya wilaya kwa huduma nzuri ambazo zimesaidia kuokoa maisha yake na watu wengine.

Salum Jawabu mkazi wa Mchuruka aliyemaliza dawa za kifua kikuu na kupoma,amewaomba watu waliobainika kuwa na TB na kuanzishiwa matibabu kuendelea kumeza dawa badala ya kukimbia kwani kufanya hivyo ni hatari kwa maisha yao.

Alisema,ugonjwa huo unatibika kwa mgonjwa kumeza dawa kila siku na kuepuka kukimbilia kwa waganga wa tiba asili na tiba ambao hawana vipimo na tiba sahihi za ugonjwa wa kifua kikuu.

## C.MKOA WA RUVUMA ULIVYODHAMIRIA KUPUNGUZA UDUMAVU NA UTAPIAMLO



KATIBU Tawala Mkoa wa Ruvuma Ndugu Stephen Ndaki ameongoza kikao cha Kamati ya Lishe Mkoa ambacho kimelenga kupokea majukumu na viashiria vya kupima utendaji kazi wa Kamati ili kupunguza udumavu na utapiamlo.

kikao hicho kilichofanyika kwenye ukumbi wa Mipango Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma pia kimepokea taarifa ya utekelezaji wa mkataba wa Lishe kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2022.

Akizungumza kwenye kikao hicho Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma amelitaja chimbuko la mkataba wa lishe unaotekelezwa katika ngazi zote,kuwa umetokana na utafiti ambao ulifanyika mwaka 2017 ambao ulibaini mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ukiwemo Mkoa wa Ruvuma iliyoongoza kwa udumavu.

“Tulikuwa tunajiuliza mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ndiyo inaongoza kwa uzalishaji wa vyakula vya aina zote sasa tukawa tunajiuliza chakula ni kingi tumedumaa vipi’’,alisema Ndaki.

Amesema wakati utafiti huo umefanyika Mkoa wa Ruvuma kwenye udumavu ulikuwa na asilimia 42 ya udumavu hivyo kuwa juu ya udumavu wa kitaifa ambao ni asilimia 39.

Hata hivyo amesema Mkoa umekuwa unachukua hatua mbalimbali za kupunguza kiwango cha udumavu ambapo umefanikiwa kupunguza kiwango cha udumavu kwa asilimia moja kutoka asilimia 42 hadi 41 kiwango ambacho amesema bado kipo juu.

Amesisitiza kuwa udumavu unapowakumba Watoto chini ya miaka mitano unaathiri hadi ukuaji wa ubongo hivyo ametoa rai kwa wajumbe wa Kamati ya Lishe Mkoa wa Ruvuma kila mmoja kuwajibika kwenye eneo lake ili kutoa elimu endelevu itakayosaidia kupunguza udumavu na utapiamlo katika Mkoa na Taifa kwa ujumla.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dr.Luois Chomboko akizungumza kwenye kikao hicho amesema ili kukabiliana na changamoto ya udumavu tangu mwaka 2017,serikali iliamua kutoa mkataba wa utekelezaji wa afua za lishe.

Amesisitiza kuwa mikataba hiyo imekuwa inatekelezwa na kwamba Septemba 30,2022,mkataba wa lishe awamu ya pili umesainiwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan ambao unatekelezwa katika ngazi za mikoa na Halmashauri.

“Lishe ni msingi wa uchumi na maendeleo na afya ya binadamu,tupo katika utekelezaji wa Mpango Mkakati Jumuishi wa pili wa Taifa wa Lishe unaoanzia mwaka 2021 hadi 2026’’,alisema Dr.Chomboko.

Hata hivyo amesema serikali imeahidi kuchangia asilimia 10.5 ya utekelezaji wa mpango huo ambao ni sawa na shilingi bilioni 67.22 katika utekelezaji na kwamba fedha hizo zitakuwa zinatoka katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Mkoa.

Kwa upande wake Mratibu wa Lishe Mkoa wa Ruvuma Neema Mtekwa amesema katika kukabiliana na utapiamlo na udumavu,Mkoa umetoa maelekezo kwa wakurugenzi ili elimu ya lishe iendelee kutolewa kwa jamii na Taasisi.

Mtekwa amesema shule zote zimeelekezwa kutumia unga ulioongezwa virutubisho,kulima mahindi na maharage lishe ili kuongeza upatikanaji wake na kwamba kupitia kikao cha Mkoa wazabuni wameelekezwa kupeleka mahindi lishe shuleni.

Kutokana na hali ya lishe na udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano kuwa mbaya nchini,Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan,aliagiza kuwepo kwa mkataba wa usimamiaji wa shughuli za Lishe baina yake na Wakuu wa Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

## D.WATU ZAIDI YA 63,000 RUVUMA WANAISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI



MKOA wa Ruvuma kwa mwaka 2022 unakadiriwa kuwa na zaidi ya watu 63,088 wanaoshi na Virusi vya UKIMWI.

Haya yamesemwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dr.Lous Chomboko wakati anatoa taarifa kuhusu ugonjwa wa UKIMWI kwenye maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani ambayo kimkoa yamefanyika Kata ya Luwaita wilayani Mbinga.

Dr.Chomboko amebainisha kuwa kati ya watu hao wanawake ni 37,233,wanaume ni 22,849 na Watoto ni 3,008.

“Kaulimbinu ya siku ya UKIMWI Duniani Desemba Mosi ni Imarisha usawa,kauli hii imelenga usawa katika ngazi za familia kwa kutokuwatenga watu wanaopata maambukizi’’,alisisitiza Dr.Chomboko.

Mganga Mkuu wa Mkoa ameutaja Mkoa wa Ruvuma kuwa ni miongoni mwa mikoa ambayo kiwango cha maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na UKIMWI kipo juu zaidi ya kiwango cha kitaifa.

Amesema kiwango cha maambukizi ya VVU na UKIMWI mkoani Ruvuma ni asilimia 5.6 ambapo kiwango cha kitaifa ni asilimia ni asilimia 4.7.

Hata hivyo amesema kiwango hicho cha maambukizi kimkoa kimepungua kwa asilimia 1.4 kutoka asilimia saba hadi 5.6 kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa viashiria vya UKIMWI na malaria kwa mwaka 2011 hadi 2012.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo ya siku ya UKIMWI Duniani,Mgeni rasmi Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas ambaye aliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbinga Mheshimiwa Aziza Mangosongo,amesisitiza jamii nzima kuwajali watu wenye VVU na UKIMWI.

Amesema licha ya jitihada zote za mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI hali ya maambukizi katika Mkoa wa Ruvuma sio nzuri kwa sababu kiwango cha maambukizi kimkoa ni kikubwa zaidi ya kiwango cha maambukizi kitaifa.

“Hivyo basi inatulazimu kuendelea kujikumbusha juu ya mikakati ya mapambano dhidi ya UKIMWI ili kuendelea kupunguza maambukizi ya VVU katika Mkoa wetu’’,alisisitiza Kanali Thomas.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma Bakari Mketo amewapongeza wadau wa afya mkoani Ruvuma kwa kuendelea kutoa huduma mbalimbali zinazosaidia kupunguza maambukizi mapya ya VVU ikiwemo tohara na uhamasishaji wa kupima VVU hali iliyosababisha asilimia 98.8 ya watu wanaoishi na VVU mkoani Ruvuma kujua hali zao.



## E.MADAKTARI BINGWA KUTOKA CHINA WALIVYOTOA HUDUMA ZA KIBINGWA BURE SONGEA




Baadhi ya madaktari bingwa kutoka nchini China ambao wanaendesha zoezi la utoaji matibabu bure kwa siku tatu kwenye uwanja wa Majimaji mjini Songea .Madaktari hao walitoa huduma za kibingwa kuanzia Novemba nane hadi kumi mwaka 2022.

Wananchi mkoani Ruvuma walijitokeza kupima afya zao na kupata ushauri wa kitaalam wa magonjwa mbalimbali.

matibabu hayo yalitolewa kwa ushirikiano wa madaktari bingwa kutoka Nchi ya China kwa kushirikiana na madaktari wa Manispaa na kutoka Hospitali ya Mkoa

## F.HUDUMA YA AFYA TA UZAZI NA MTOTO MKOANI RUVUMA



Vituo vinavyotoa huduma ya Afya ya Uzazi na mtoto vimeongezeka kutoka 324 hadi 348 sawa na asilimia (98%) ya vituo vyote vinavyotoa huduma katika Mkoa. Kati ya vituo vinavyotoa huduma ya afya ya uzazi na mtoto, Vituo 316 sawa na asilimia 92 vinatoa huduma ya chanjo. Aidha kati ya vituo vya afya 36, vituo 14 (38.8%) ya vituo vya Afya (H/C) vinatoa huduma kabambe za dharura za mama wajawazito na Watoto wachanga (CEmONC).

Kwa upande wa huduma ya wazazi, kiwango cha akina mama waliojifungulia kituoni kimeongezeka kutoka asilimia 84.4 mwaka 2020 hadi asilimia 85.4 Desemba 2021. Kiwango hiki ni juu ya lengo la taifa la asilimia 80.

Idadi ya vifo vya wazazi vimepungua kutoka vifo 24 Disemba mwaka 2021 hadi vifo 20 sawa na vifo 39 /100,000 vizazi hai Novemba mwaka 2022.

Sababu zilizochangia vifo ni Kutokwa na damu nyingi PPH, Kifafa cha mimba, mgando katika mishipa ya damu (Embolism), Upungufu wa damu na madhara ya dawa za usingizi (anaethetic complication).

Vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja kwa mwaka 2022 vimepungua kutoka 131 sawa na vifo 3 kati ya watoto 1000 waliozaliwa hai mwaka 2021 hadi vifo 88 sawa na vifo 2 kati ya watoto 1000 waliozaliwa hai Disemaba mwaka 2022. Sababu zilizochangia vifo hivyo ni magonjwa ya watoto wachanga (perinatal condition). Vifo 35 sawa na asilimia 40.0 Prematurity vifo 25 sawa na asilimia 28.4, Pneumonia vifo 13 sawa na asilimia15.0, Malaria vifo 7 sawa na asilimia 8.0, Septicemia vifo 5 sawa na asilimia 6.0 na Anaemia vifo 3 sawa na asilimia 3.4 ya vifo vyote.

Takwimu za vifo vya watoto chini ya miaka mitano vilivyotolewa taarifa ngazi ya vituo na jamii kwa mwaka 2022 vilikuwa 124 sawa na vifo 3 kati ya watoto 1000 waliozaliwa hai. Idadi ya vifo hivi imepungua ukilinganisha na vifo 204 sawa na vifo 4 kati ya watoto 1000 waliozaliwa hai mwaka 2021. Sababu zinazoongoza kwa vifo hivyo ni Neonatal condition vifo 41 sawa na asilimia 33.0, Pneumonia vifo 33 sawa na asiimia 26.6 malaria vifo 24 sawa na asilimia 19.3, Septicaemia vifo 15 sawa na asilimia 12.0 na Anaemia vifo 11 sawa na asilimia 9.0 ya vifo vyote.

Katika kipindi cha Januari hadi Novemba, 2022 Mkoa umekuwa na mafanikio makubwa katika utoaji wa huduma za chanjo mbalimbali kama ifuatavyo;

Chanjo ya kifua kikuu (BCG) ni 141%, chanjo ya kuzuia kupooza (Polio) 125%, chanjo ya Donda koo, kukakamaa na kifaduro (DTP3) 123% chanjo ya kuzuia homa ya mapafu (Pneumonia) 122%, chanjo ya kuzuia kuharisha

(Rota virus) 99.5%, chanjo ya surua (Measles Rubella) 122%, chanjo ya Pepopunda (Td) kwa wajawazito 117% na chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi (HPV) kwa wasichana wenye umri wa miaka 14 ni 115%.

Mkoa umeendelea kutoa chanjo ya ugonjwa wa Korona ikiwa ni jitihada za kupambana na ugonjwa huu ambapo kwa kipindi cha kuanzia tarehe 04 Agosti, 2021 hadi tarehe 31 Oktoba, 2022 jumla ya watu 1,045,390 wamekamilisha dozi ya chanjo ya korona sawa na asilimia 109. Mkoa uliwekewa kuchanja jumla ya watu 670,577 ambao ni sawa na asilimia 70 ya watu wote wenye umri wa miaka 18 na kuendelea (ambao ni 957,938).

Mkoa wa Ruvuma umeongoza Kitaifa kwa utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 na kupewa vyeti 2 na tuzo kwa vipindi tofauti tofauti kwa mwaka 2021 hadi Mei, 2022. Pia katika mazoezi ya Kitaifa ya utoaji wa chanjo ya polio Mkoa wa Ruvuma umefanya vizuri katika awamu zote 4 (awamu ya kwanza nay a pili Tuliongoza Kitaifa iliyofanyika mwezi Machi na Mei, 2022). Utoaji wa chanjo za kawaida tunaendelea kufanya vizuri tangu tutangazwe kuwa vinara 2021.



## H.HUDUMA YA LISHE KATIKA MKOA WA RUVUMA



***Pichani ni wajumbe wa Kamati ya Lishe mkoani Ruvuma***

Katika kuendelea na kupambana na tatizo la utapiamlo nchini hususani udumavu, Mkoa wa Ruvuma unatekeleza viashiria mbalimbali vilivyoainishwa katika mkataba wa Lishe ulioingiwa baina ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma. Utekelezaji wa mkataba kwa mwaka 2020/2021 Mkoa wa Ruvuma ulikuwa ni mshindi wa pili kitaifa na mwaka 2021/2022 Mkoa umeshika nafasi ya 4 Kitaifa. Matokeo haya kwa kiasi kikubwa yametokana na; -

- ✓ Matumizi ya Kifungu/Lengo Y (Objective Y) katika kutekeleza shughuli zisizo za Lishe.
- ✓ Kutumia vifungu/malengo mengine (objectives) kutekeleza shughuli za Lishe.

Haya yote yaliyotajwa hapo juu yamesababisha Mkoa kutofanya vizuri katika utekelezaji wa Mkataba wa Lishe katika mwaka wa fedha 2021/2022. Hivyo, ili kutekeleza Mkataba wa Lishe kwa Kiwango kinachotakiwa tunapendekeza yafuatayo; -

- ✓ Waweka hazina wa Halmashauri wahakikishe vifungu vya Lishe (Objective Y expenditure codes) vinatumika kulipia shughuli za lishe tu
- ✓ Maafisa Mipango wahakikishe vifungu vya Lishe vinatumika kupanga shughuli za Lishe tu
- ✓ Maafisa Lishe wa ainishe vifungu sahihi vya shughuli anayokwenda kutekeleza.
- ✓ Wakaguzi wa ndani ya Halmashauri wahakikishe wanafanya uhakiki wa fedha za lishe kila robo mwaka ili kubaini changamoto mapema na kuzitatua kwa wakati.

Aidha, katika mwaka wa fedha **2022/2023** Mkoa kupitia Halmashauri zake umeendelea kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo utengaji na utoaji wa fedha kwa ajili kutekeleza afua za lishe, ambapo jumla ya **TZS. 355,274,918.3** zimepangwa na hadi kufikia Novemba, 2022 jumla ya **TZS. 122,852,599** sawa na asilimia **34.6 tu** zimetolewa kutekeleza afua za lishe katika Halmashauri kama inavyoonesha katika jedwali namba 50.

**Jedwali linaonesha Matumizi ya fedha zilizopangwa kutekeleza afua za lishe kwa Halmashauri katika mwaka wa fedha 2022/2023**

| NA | HALMASHAURI | FEDHA ILIYOTUMIKA JULAI - NOVEMBA, 2022 IKILINGANISHWA NA FEDHA ILIYOPANGWA MWAKA 2022/2023 | | | KIASI CHA FEDHA KILICHOPANGWA KWA MTOTO (PER CAPITA PLANNED) FY 2022/2023 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | KILICHOPANGWA | KILICHOTUMIKA HADI NOVEMBA, 2022 | % | IDADI YA WATOTO | TZS |
| 1 | SONGEA MC | 39,860,000 | 24,404,000 | 61.2 | 32216 | 1237 |
| 2 | MBINGA TC | 23,971,068 | 7,526,000 | 31.4 | 20961 | 1144 |
| 3 | SONGEA DC | 38,729,712 | 6,570,000 | 17.0 | 21396 | 1810 |
| 4 | MBINGA DC | 92,711,750 | 37,140,000 | 40.1 | 41575 | 2230 |
| 5 | TUNDURU DC | 71,204,134 | 21,254,600 | 29.9 | 47833 | 1489 |
| 6 | NAMTUMBO DC | 39,432,000 | 5,070,000 | 12.9 | 36712 | 1074 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 7 | NYASA DC | 23,823,206 | 11,744,000 | 49.3 | 27023 | 882 |
| 8 | MADABA DC | 25,543,048.3 | 9,143,999 | 35.8 | 7684 | 3324 |
| **JUMLA KUU** | | **355,274,918.3** | **122,852,599** | **34.6** | **235400** | **1509** |

**NB:** - Halmashauri **saba (7)** ziliweza kupanga kwa kufuata kigezo cha kima cha chini cha **TZS. 1000** kwa kila mtoto chini ya miaka mitano, isipokuwa ***Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa*** ambayo ina jumla ya Watoto wenye umri chini ya miaka mitano **27023** lakini wamepanga **TZS. 23,823,206** badala ya kima cha chini cha **TZS. 27,023,000**. Athari ya hii itafanya Halmashauri kutofikia matumizi ya kima cha chini cha **TZS. 1000** wakati wa tathmini na mwisho wa siku itaathiri matokea ya Mkoa Kitaifa.

**Mambo yanayosababisha lishe duni ni: -**

i. Ulaji duni wa chakula unaotokana na kula milo michache na kiasi kisichotosheleza mahitaji ya virutubishi mwilini, hii pia hujumuisha kutowanyonyesha watoto ipasavyo.

ii. Magonjwa ya mara kwa mara yanayoondoa hamu ya kula na, kusababisha ufyonzaji duni wa virutubishi na huongeza mahitaji ya virutubishi mwilini.

iii. Matumizi mabaya ya chakula mfano kuuza chakula chote, kutumia nafaka kutengenezea pombe nk.

iv. Utayarishaji mbaya wa chakula unaopoteza virutubishi kama kuosha mboga za majani baada ya kukatakata.

v. Upungufu katika matunzo ya makundi maalumu (watoto wadogo, wanawake wajawazito na wanaonyonyesha, wazee na wagonjwa) Makundi haya yanahitaji matunzo na huduma muhimu za kiafya kama vile chanjo, kupata vidonge vya nyongeza, kutibu maradhi na huduma za kilishe.

Utapiamlo huathiri afya, uzalishaji mali na maendeleo katika jamii. Athari hizi hujitokeza katika hali ya kuchelewa kwa hatua za ukuaji wa mtoto kimwili na kiakili, kuongezeka kwa magonjwa na vifo vya watoto, kupungua kwa kinga mwili na kupungua kwa uwezo wa kufanya kazi za uzalishaji mali.

Hivyo, katika kuhakikisha jamii inaondokana na tatizo hili la lishe Halmashauri na Mkoa ni muhimu kuendelea kuelekeza nguvu katika kusimamia utekelezaji wa mikataba ya lishe ngazi ya Halmashauri, kata na vijiji / Mitaa ili jamii iweze:-

a) kubadili tabia na kuzingatia ulaji unaofaa.
b) Kupata elimu sahihi ya lishe kwa kupitia njia mbalimbali kama vyombo vya habari vilivyopo, ngoma za asili, viongozi wa dini na kimila.
c) Kupata elimu sahihi ya lishe katika kipindi cha siku 1000 za uhai wa mtoto (yaani toka mimba ilipotungwa hadi mtoto anapofikisha umri wa miaka 2) –
d) Kuimarisha maadhimisho ya siku za afya na Lishe ya Kijiji zinazofanyika kila baada ya miezi mitatu.
e) Mkoa na Halmashauri kuhakikisha fedha inayotengwa kwa shughuli za lishe inatolewa na kufanya shughuli za lishe kama zilivyotengwa.
f) Mkoa na Halmashauri kuendelea kufanya usimamizi shirikishi ili kuweza kutambua changamoto zinazojitokeza kwa wakati na kuzitafutia ufumbuzi.

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**OFISI YA MKUU WA MKOA WA RUVUMA**

**1 BARABARA YA TUNDURU**

**S.L.P 74 SONGEA**

**57180 RUVUMA**
**SIMU Nambari.025- 2602256/2602238**
**FAX Na.2602144**
**E-MAIL:** ras.ruvuma@tamisemi.go.tz
**TOVUTI:www.ruvuma.go.tz**
**INSTAGRAM; kusini_News**

**FACEBOOK: kusini_News**

**TWITTER:kusini_News**

**YOU TUBE;kusini News**